ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	**-**	**SPIKA**
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi

8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa

		Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais
19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera
22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni

23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake
28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe. Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe

32. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil	-	Uteuzi wa Rais
33. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
34. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
35. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
36. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
37. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
38. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
39. Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani
40. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Nafasi za Wanawake
41. Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Jimbo la Wawi
42. Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Nafasi za Wanawake
43. Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Jimbo la Shaurimoyo
44. Mhe. Hassan Khamis Hafidh	-	Jimbo la Welezo
45. Mhe. Hidaya Ali Makame	-	Nafasi za Wanawake
46. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)	-	Jimbo la Mtoni
47. Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	Jimbo la Paje
48. Mhe. Khadija Omar Kibano	-	Jimbo la Mtambwe
49. Mhe. Machano Othman Said	-	Jimbo la Mfenesini
50. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti	-	Jimbo la Mtopepo
51. Mhe. Makame Said Juma	-	Jimbo la Kojani
52. Mhe. Maryam Thani Juma	-	Jimbo la Gando

53. Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu

54. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni

55. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile

56. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae

57. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini

58. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini

59. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake

60. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole

61. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani

62. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake

63. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake

64. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani

65. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani

66. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni

67. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde

68. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

69. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni

70. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake

71. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi

72. Mhe. Said Hassan Said - Mwanasheria Mkuu

73. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Nafasi za Wanawake

74. Mhe. Salma Mussa Bilal	-	Nafasi za Wanawake
75. Mhe. Shaib Said Ali	-	Jimbo la Chonga
76. Mhe. Simai Mohammed Said	-	Jimbo la Tunguu
77. Mhe. Sira Ubwa Mamboya	-	Uteuzi wa Rais
78. Mhe. Suleiman Makame Ali	-	Jimbo la Ziwani
79. Mhe. Suleiman Sarahan Said	-	Jimbo la Chakechake
80. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
82. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
85. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
86. Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem	-	Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Kumi na Nne – Tarehe 26 Februari, 2018

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe Spika (Zuberi Ali Maulid) alisoma Dua

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe katika Kikao cha Baraza cha tarehe 20 Februari, 2018, Mhe. Omar Seif Abeid aliuliza swali la nyongeza kwa Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora linalotokana na swali la msingi Nam. 38. Sasa namuomba Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora asome jibu la swali la nyongeza lililoulizwa na Mjumbe huyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kutoa jibu la maandishi lililotokana na swali la nyongeza la Mhe. Omar Seif Abeid, Mwakilishi wa Jimbo la Konde wakati nilipokuwa nikimjibu swali la msingi Namba 38 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, mashamba manne (4) yaliyokuwa Pemba ni shamba la Bwana Ahmed Said Baziadi liliopo Bwagamoyo Mtambwe, Shamba la Bi. Suria Binti Khamis liliopo Kivumoni Chonga, Shamba la Mskiti wa "*Hanafy Mosque"* liliopo Kwale Mpona Micheweni na Shamba la Bwana Muhammed Mabrouk "UTBI" liliopo Mgagadu Mkoani.

Mhe. Spika, kwa heshima naomba kuwasilisha.

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Rashid Makame Shamsi (Mwenyekiti wa Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo): Mhe. Spika, naomba sasa kuwasilisha Hati Mezani ya Ripoti ya Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo ya Mwaka 2017/2018.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 55

Changamoto za Ajira kwa Vijana

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza:

Kwa kuwa moja kati ya vipaumbele vya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto kwa mwaka wa fedha unaoishia June, 2018 ni kuhakikisha kwamba inasimamia ipasavyo Sheria ya Kazi na Ajira kwa Vijana na kwa sababu vijana ndio nguvu kazi ya Taifa lolote duniani.

(a) Je, ni ipi hatua ya utekelezaji iliyofikiwa hadi sasa ili kuhakikisha kwamba vijana wetu wanapatiwa ajira au kuwezeshwa kujiajiri wenyewe na kupunguza pengo la idadi ya vijana wasiokuwa na kazi hapa Zanzibar.

(b) Je, kwa mwaka 2017/2018 hadi kufikia Disemba, 2017, ni vijana wangapi ambao wameshapatiwa ajira kupitia Wizara husika au ni vijana wangapi ambao wamewezeshwa kujiajiri wenyewe kupitia mpango huu.

(c) Je, ni waajiri wangapi waliobainika kuwanyanyasa wafanyakazi wao na malalamiko mangapi ya uvunjifu wa Sheria za Kazi yaliyoripotiwa kwa Taasisi mbali mbali na ni hatua gani zilizochukuliwa dhidi ya Waajiri hao ili kukomesha tabia ya baadhi ya waajiri kuwanyanyasa na kuwanyanyapaa wafanyakazi wao.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto - Alijibu:

Mhe. Spika, awali ya yote kwanza naomba niendelee kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehma ambaye na yeye anaendelea kutupa pumzi zake na tukaweza kukutana asubuhi hii katika Baraza lako tukufu tukiwa na wenye afya njema.

Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu sasa kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 55 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, katika kuhakikisha kuwa vijana wetu wanapata ajira, Wizara kupitia Idara ya Ajira inaendelea kutoa mafunzo mbali mbali yanayohusu Ajira, miongoni mwa mada ambazo hutolewa ni umuhimu wa ajira na kujiajiri, namna bora ya kushinda kwenye usaili, sifa za mwenye kuajiriwa na mahitaji ya muajiri kwa muajiriwa.

Kwa kipindi cha Julai hadi Disemba 2017 vijana 400 kwa Unguja wamefaidika na mafunzo hayo na kwa Pemba jumla ya vijana 150 wamefaidika. Vile vile Wizara inaendelea kutekeleza mradi wa majaribio kwa wanagenzi ili baadae waweze kuajirika au kujiajiri. Hadi kufikia Disemba 2017 jumla ya vijana 52 bado wanaendelea na mafunzo hayo katika Chuo cha Utalii Maruhubi.

Vile vile Wizara inaendelea na utafiti kwa kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ili kubaini fursa zilizopo katika sekta ya Kilimo na Uvuvi ili baadae serikali iweke mikakati ya kuweza kufaidika nazo kikamilifu. Pia wizara inaendelea kushirikiana na Kamati za Kisekta za Uzalishaji Ajira za Wilaya ili kuona na kuibua fursa katika ngazi za Wilaya.

b) Mhe. Spika, kwa mujibu wa taarifa tulizozikusanya kwa kipindi cha Juali - Disemba vijana 652 wamepata ajira katika sekta binafsi. Kati ya hao vijana 629 ni kwa upande wa Unguja na 23 kwa upande wa Pemba. Ajira hizo ni kutoka mahoteli mbali mbali na Taasisi nyengine za binafsi.

c) Mhe. Spika, serikali kupitia Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto imeweza kuwabaini waajiri 11 ambao wamebainika kuwanyanyasa wafanyakazi wao na hatua mbali mbali zimechukuliwa.

Mhe. Spika, vile vile mashauri 91 yaliripotiwa katika Kitengo cha Usuluhishi na Uamuzi wa Migogoro ya Kazi, kati ya hayo 47 yamesuluhishwa, 31 yameamuliwa na 13 bado yanaendelea katika usuluhishi.

Hata hivyo kupitia Maafisa Kazi wa Mikoa, Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, wanawake na Watoto inaendelea kupokea malalamiko kadhaa katika shughuli zake za kila siku ambayo yanashughulikiwa kwa kutolewa ushauri unaofaa kwa waajiri na kuchukuliwa hatua kila inapobidi.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Spika, namshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu mazuri yenye muelekeo wa wizara lakini pia naomba kuuliza kwa kuwa pengo la uajiri ni kubwa liliopo hapa kati ya vijana wetu wa Unguja na Pemba ambao wameelekeza vijana wetu Wakizanzibari na wale wanaotoka nje. Na kwa kuwa kumeelezwa hapa ni vijana 652 tu ambao wameajiriwa wa Kizanzibari.

Je, kunautaratibu gani ambao umepangwa wa kisheria kuhakikisha kwamba hizi nafasi nyingi za mahoteli, ukiachilia zile za kitaalamu ambazo vijana wetu hawaziwezi, zinakuja kwa vijana wetu wa Zanzibar kulikono kutoka nje ya Zanzibar. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo:

Mhe. Spika, kama nilivyosema Wizara yetu ina mikakati ya kuhakikisha kwanza kupita katika Mahoteli na kuhakikisha kwamba zile nafazi ambazo Wazanzibari wana ujuzi nazo na wanaweza kuzifanya, basi tuhakikishe kwamba nafasi zile zote wanapewa wazawa. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Spika, nikushukuru sana kwa kuniona. Nichukue nafasi hii kwanza nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri lakini pia nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kauli ya juzi aliyoitoa kuhusiana katika Mkutano wa Jumuia ya Afrika Mashariki kwamba hakuna jambo lolote ambalo linamtafaruku baina ya Kenya na Tanzania. Naamini itakuwa ni fursa nzuri kwa wafanyakazi wetu wa Zanzibar hasa kwa Mhe. Suleiman Sarahan Said kuhakikisha kwamba tunapata usafiri wa baharini baina ya Mombasa, Pemba na Unguja.

Mhe. Spika, naomba kuuliza swali dogo tu la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri naomba unisikilize vizuri, kwa kuwa kwenye kifungu Nam. 13 au ibara ya Nam. 13 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (2), inasema:-

13(2) Ni marufuku kwa sheria yoyote iliyotungwa na mamlaka yoyote katika Jamhuri ya Muungano kuweka sharti lolote ambalo ni la ubaguzi ama wa dhahiri kwa taathira yake."

Lakini namba 4 pia hiyo hiyo inasema:

13(4)Ni marufuku kwa mtu yeyote kubaguliwa na mtu wa mamlaka yoyote inayotekeleza madaraka yake chini ya sheria yoyote katika utekelezaji wake wa kazi au shughuli yoyote ya Mamlaka ya Nchi.

Mhe. Naibu Waziri ni utaratibu gani Wizara yako imejiwekea katika kuhakikisha kwamba Wazanzibari ambao wanafanya kazi ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hasa kwa upande wa Tanzania Bara hawabaguliwi na kazi zao na kazi zao za shughuli zao za kila siku.

Lakini halikadhalika ni utaratibu gani au njia gani ambayo Wizara yako hasa kwa upande wa Zanzibar unahakikisha kwamba Wazanzibari na ndugu zetu kutoka Tanzania Bara wanapokwenda kufanya kazi katika maeneo tofauti inakuwa fursa ni sawa, haki itendeke pale kutokana na uwezo, juhudi na elimu waliyokuwa nayo.

Je, Wizara yako imejipangaji katika mikakati katika sehemu zote mbili za muungano kuhakikisha kifungu hichi cha Katiba hakiendi kinyume.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, ahsante kwanza nimshukuru Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto, kwa kuweza kujibu vizuri. Pamoja na majibu mazuri na swali la Mhe. Mjumbe naomba nijibu kama hivi ifuatavyo:

Naomba niseme tu kwamba hakuna ubaguzi wowote unaofanyika kati ya Tanzania Bara na Visiwani. Wanapokuja kusailiwa, wakisailiwa na sifa wanazo, nafasi za mwanzo kama ni Zanzibar wanapewa watu wa Zanzibar. Kinachoamua pale ni uwezo wa kazi na mahitaji na nafasi zilizokuwepo mahali pale. Mpaka sasa hivi hatujapata malalamiko yoyote yanayohusiana na masuala ya ubaguzi wanapokwenda kuomba ajira. Ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii kuweza kuuliza swali dongo la nyonge lenye vifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:

Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali la nyongeza.

a) Mhe. Waziri katika majibu yake umesema kwamba kuna vijana wamepewa taaluma wakiwemo Pemba na Unguja, nikitaka kujua ni taaluma ya aina gani waliyopewa ya kibiashara. Ninavyofahamu kuna ongezeko la thamani ambalo ni *value addition*, pamoja na taaluma ya masoko pamoja na taaluma nyengine, nikitaka nijue ni taaluma gani waliyopewa vijana hawa ili kuhakikisha wanajitikita katika biashara.

b) Lakini pia vile vile juzi katika ripoti zao za Kamati, Kamati ya Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) ilisema kwamba changamoto kubwa ni kuajiriwa vijana wazalendo katika mahoteli. Leo tunapata majibu kwamba vijana mia sita na zaidi wameajiriwa katika mahoteli, nikitaka kujua ni hoteli aina gani au ni hoteli gani, na ni Wilaya ngapi ambazo vijana hawa wanatoka ili kupata kujua ukweli uko wapi.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Mhe. Spika, kama nilivyosema katika majibu yangu mama kwamba Wizara inatoa majaribio ya kuwawezesha mafunzo wanayopewa ya kuwawezesha kujitambua wakati wa kujiajiri au kuajiriwa wanayopewa.

b) Suala lake analosema anataka kufahamu kwamba hao vijana 600 ni wa Wilaya zipi na hoteli zipi. Kwa suala lake hili kwa sababu linataka takwimu namuomba Mhe. Mwakilishi niweze kumjibu kwa maandishi. Ahsante.

Nam. 66

Utaratibu wa Uendeshaji wa Skuli za Binafsi

Mhe. Suleiman Sarahani Said - Aliuliza:

Baada ya Serikali kuruhusu skuli binafsi, kumekuwa na changamoto kwa baadhi ya skuli hizo kutofuata na kutii maagizo ya mwenendo wa mfumo wa elimu kwa madhumuni ya kuleta ufanisi katika elimu, kudumisha maadili, utamaduni na silka za Zanzibar.

(a) Ni kwa nini skuli za Serikali na za binafsi hazifungwi kwa wakati mmoja ili kuondoa usumbufu kwa wazee.

(b) Ni kwa nini skuli za binafsi hazisomi nyimbo za wanafunzi zilizowekwa na Serikali hasa asubuhi wakati wa paredi.

(c) Je, Serikali haioni kutokuziwekea skuli za binafsi mikakati ya kufuatwa kisheria ndio kutoa mwanya wa skuli hizo kufanya wanayoyataka.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suala lake Nam. 66 lenye vipengele (a), (b) na (c), kwanza napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Skuli zote za Serikali na za binafsi zinapaswa kisheria kufuata miongozo na maelekezo yanayotolewa na Wizara kuhusu uendeshaji na usimamizi wa skuli. Wizara kwa kutumia Ofisi ya Mrajis wa Elimu na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu inazifuatilia skuli zote binafsi ili kuhakikisha kuwa zinafuata maadili ya utamaduni na silka zetu kama zinavyotakiwa.

Baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu kama ifuatavyo:-

a) Wizara inaushirikisha umoja wa skuli za binafsi Zanzibar *"Zanzibar Association of Private School (ZASP)* katika kupanga ratiba ya kufunga na kufungua skuli kwa madhumuni ya kuhakikisha kuwa skuli zote za Serikali na za binafsi zinafungwa na kufunguliwa kwa wakati mmoja. Skuli ambayo

haifuati ratiba ya kufungua na kufunga skuli iliyotolewa na Wizara itakuwa inafanya kosa na Wizara itakapoigundua itaichukulia hatua za Kisheria.

b) Wizara imetoa mwongozo kuhusu nyimbo za dua ambazo wanapaswa kusoma wakati wanapofika skuli na kusimama pamoja kabla ya kuingia madarasani. Wizara haina taarifa rasmi ya skuli ambazo hazifuati maelekezo ya muongozo lakini itazifuatilia kuhakikisha kuwa zinatekeleza maelekezo ya Wizara.

c) Wizara imeanza taratibu ya kuiangalia upya Sheria ya Elimu Namba 6 ya mwaka 1982 na itapendekeza marekebisho ya baadhi ya vifungu vya Sheria hiyo ili ioane na mahitaji na mazingira ya sasa ikiwemo vifungu vinavyohusiana na usajili na uendeshaji wa skuli za binafsi.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nakushukuru sana Mhe. Spika, na mimi nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini nimuulize Mhe. Naibu Waziri kwenye swali la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

Mhe. Simai Mohamed Said: Kidogo sauti yako inaingia huku inamchanganya Mhe. Naibu Waziri. Tuendelee Mhe. Suleiman Sarahan.

a) Mhe. Naibu Waziri tokea kuingia madarakani je, umeshawahi kuzitembelea skuli binafsi na ukazifanyia mikutano ili kujua matatizo yao au kujua utaratibu wao.

b) Wewe ulitoa tamko la kwamba skuli zote zipachike bendera katika skuli zao, umeshazikagua skuli zote na kuhakikisha zimepachikwa bendera na kama kuna skuli ambayo haijapachika bendera nini adhabu yake.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda nimjibu Mhe. Mwakilishi maswali yake ya nyongeza kama hivi ifuatavyo:

a) Mimi kama Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali tayari nimeshatembelea baadhi ya skuli, lakini pia nimeshawahi kufanya mikutano na Jumuiya yao ya *Private School* na kuelekezana baadhi ya mambo yanayohusu elimu.

b) Pia kwa upande wa bendera mimi binafsi yangu imeshafanya ziara ya kukagua skuli nyingi na kuona kwamba wanapachika bendera au laa. Nyingi au zote zile ambazo nimewahi kuzitembelea tayari zimepachika bendera hizo.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante sana Mhe. Spika, naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri wa Elimu kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, skuli binafsi utafiti unaonyesha kwamba zinafanya vizuri kuliko skuli za serikali. Je, wizara ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba skuli za serikali zinafanya vizuri kuliko skuli binafsi.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Ni kwamba si sahihi sana kutoa kauli kama hiyo kwa sababu kuna ngazi nyengine za mitihani skuli za serikali zinaongoza kuliko za binafsi na kuna ngazi nyengine skuli za *private* zinaongoza zaidi kuliko skuli za serikali.

Hata hivyo sasa hivi Wizara imejipanga na inaendelea kujipanga kwa kuzipatia skuli hizo walimu wa kutosha hasa wa masomo ya sayansi. Hivi sasa Wizara inaendelea kuajiri lakini pia tutapata walimu wa kusaidia katika masomo ya *physics* na *mathematics* hivi karibuni wakati wowote kuanzia sasa kutoka Nigeria.

Lakini pia mkakati mwengine ni kuongeza bajeti kwa ajili ya vifaa vya maabara na kuongeza vitabu. Haya ni baadhi ya mikakati ambayo Wizara inachukua ili kuhakikisha kwamba ufaulu unaongezeka mwaka hadi mwaka.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa hii. Pamoja na majibu masuri aliyojibu Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mfunzo ya Amali na kwa suala zuri la msingi alilouliza Mhe. Sarahan na pamoja na vifungu alivitaja Mhe. Simai vya suala la ubaguzi. Naomba nimuulize swali la nyongeza Mhe. Waziri lifuatalo.

Kwa kuwa swali hili ninaloliuliza la suala la ubaguzi alianza kulijibu kwamba skuli za binafsi zinafuatilia suala la wanafunzi kufanya mitihani katika skuli nyengine mithani yao ya mwisho, na kwa kuwa suala hili tayari bado linaendelea na wanafunzi wameshatayarishwa kufanya skuli nyengine ambazo kuwa sizo walizosoma kufanya mitihani yao ya mwisho.

Je, hatua gani atakayochukua kuna suala hili linakemewa na linachukuliwa hatua kufanya kitihani yao ya skuli za msingi aliyoanzia kwa zile skuli binafsi ambazo kuwa zimeshawatayarisha wanafunzi hao, ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda nimjibu Mhe. Mattar suala lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Tayari wizara imeshalitolea kauli suala hili kwamba ikiwa mwanafunzi amesomeshwa katika skuli *"x",* na ikafikia wakati wa kufanya mtihani mwanafunzi huyo akabadilishwa skuli kwa maana kwamba awe *private candidate*, suala hili wizara inalipinga *hundred percent* na skuli ambayo itafanya hivyo itachukuliwa hatua na hili suala limeshatolewa kauli muda mrefu labda lirejewe tu, ahsante sana.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa kuuliza swali dogo la nyongeza kwanza nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana na inaonyesha tutafika.

Mhe. Naibu Waziri katika majibu yako ulionesha utaratibu mzuri wa kushirikiana kwa mambo mengi tu katika skuli hizi binafsi, lakini na sisi tunajua namna ya mashirikiano yenu.

a) Je, katika suala la wana taaluma maana yake ukaguzi wa wana taaluma, wizara yako katika skuli binafsi inashiriki vipi katika kuwakagua wana taaluma hawa ambao tunazungumzia wale walimu wanasomesha katika sekta binafsi kwa sababu tumewakabidhi mitaala na mambo mengine.

b) Kama haishiriki ni hatma gani pale panapotokezea makoseo hasa ya ufundishaji katika wana taaluma hawa katika skuli binafsi.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda nimjibu Mhe. Miraji kwa suala lake lake (b) kama ifuatavyo:

Napenda nieleze kwamba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kupitia Mkaguzi Mkuu wa Elimu pia inazifanyia ukaguzi skuli binafsi na inafanyia ukaguzi katika maeneo mbali mbali. Ukaguzi katika ngazi ya kuonesha kwamba skuli hizo zinakidhi vigezo vya kuanzishwa kwake au la, ukaguzi wa leseni za walimu na ukaguzi wa taaluma.

Hata inapofika mwishoni mwa mwaka huwa tunafanya ukaguzi kuangalia kiasi gani cha muhtasari imeweza kusomeshwa basi skuli za binafsi huwa tunaziingiza, ahsante sana.

Ununuzi wa Mashine ya *DNA*

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza**:**

Katika jitihada zake za kuboresha huduma za afya, Serikali ina mpango wa kununua *DNA* mashine ili kuweza kuvitambua vitu mbali mbali ambavyo sio rahisi kuvigundua kwa mashine za kawaida.

a) *DNA* mashine ambayo inataka kununuliwa hivi sasa na Wizara ya Afya ni ya kisasa kwa toleo jipya au ni *DNA* mashine ya kawaida tu.

b) Je, mashine hiyo ina uwezo wa kugundua mabaki ya binadamu aliyezikwa mpaka kwa miaka mingapi.

c) Je, mashine hiyo ina uwezo wa kugundua au kukamua majimaji ya mtu aliyebakwa kwa muda wa siku ngapi tokea kitendo kilipotokea.

Mhe. Waziri wa Afya - Alijibu**:**

Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia sote tukiwa wenye afya njema na wazima katika kutumikia majukumu tuliopewa ya kuwatumikia wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, naomba kujibu suala namba Nam 70 lenye kifungu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika**,** *DNA machine* ambayo inataka kununuliwa hivi sasa na Wizara ya Afya ni ya kisasa kabisa yaani *latest model* kwa mujibu wa toleo jipya yaani *latest version*. Mashine hiyo ina uwezo wa kugundua mpaka mabaki ya binadamu akiwa ameshazikwa hadi mifupa yake ama kile kitambaa akichofungiwa, yaani sanda basi ikichukuliwa kipande mashine hii itakuwa inaweza kugundua hivi vimelea vya *DNA*, nayo ina uwezo wa kugundua au kukamua maji maji ya mtu aliyebakwa kwa muda wa wiki moja tokea kitendo hicho kilipotokea, ikiwa yake maji maji hayakusafishwa, yaani yale maji maji yalioko sehemu ile mpaka muda wa wiki moja, baada ya wiki moja yanaweza kuwa tabu kwa mashine hii. Kwa hivyo Mheshimiwa *process* ya kununuliwa mashine hii tayari imeshaanza na hivi sasa tenda itatangazwa wakati wowote ule. Ahsante.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nakushukuru sana Mhe. Spika na mimi nimshukuru Waziri kwa majibu yake mazuri, nimuulize Waziri kwamba katika

sehemu zile ambazo amesema yeye kwamba yakibakisha mabaki yake ya maji maji katika kile kitendo anasema kwamba hata wiki moja yanaweza kufaa.

a) Lakini sehemu zile zote ni sehemu za usafi, mtu yule anakwenda haja kubwa na haja ndogo. Sasa yale maji yatabakia vipi katika sehemu ila au anatufahamisha tufanyeje katika sehemu ile.

b) Tuna mashine hii ya *DNA* ambayo inataka kuletwa lakini kwa mtazamo ni kwamba nasikia na Pemba ipo, lakini haijafanya kazi na haina daktari kweli si kweli.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

a) Nimesema yale maji maji yakiwa yamebakia sio sehemu za siri mfano yamemwagika kwenye shuka, yamemwagika juu ya kitanda ama kwenye nguo aliyovaa muhusika Yule, maji maji hayo yataweza kupimwa katika nguo hiyo ama shuka hilo, ama kitanda hicho kwa muda mpaka wiki moja yaani, yaani *investigation* yake kwa muda wa wiki moja.

b) Mashine iliyopo Pemba siyo ya *DNA*, inaitwa *Genexpert machine* hiyo tumekwenda kuiangalia baada ya Wawakilishi kuelezea pai humu ndani ya Baraza la Wawakilishi, mashine hiyo ni *Genexpert.* Kazi yake kupima hasa *TB* sugu, ile *TB* ambayo haitibiki kwa hizi dawa za kawaida inaitwa *TB* sugu, *multi-drug-resistant TB* ndio mashine hiyo inapima. Na inapima kuangalia vile virusi *strain* yaani kabila ya ile virusi ili iweze kutumia dawa husika kwa virusi hivyo, ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, nikushukuru sana miye na kwanza nitoe fursa hii kuipongeza Wizara ya Afya kwa *operation* niliyofanya juzi kwenye vichwa maji karibu sijui kama thelathini au arubaini na tumefanikiwa vizuri na kushirikiana ndugu zetu wa Australia, nipongeze sana wizara kwa kazi iliyoifanya na panapo moja tutasema moja, mbili tutasema mbili na wengine walikwenda hata India hawakufanikiwa wamefanikiwa Hospitali ya Mnazi Mmoja, ni jambo kupongezwa sana. Lakini Mhe. Waziri nikushukuru kwa leo Naibu Waziri umemuweka benchi na umekwenda mwenyewe kujibu kwa mujibu wa Kanuni zetu.(*Makofi*).

Mheshimiwa tulipewa msaada wa jenereta tena bure na kwa jitihada zako imechukua miezi sita kufunga, limekaa pale bure limechukua karibu miezi sita mpaka tukahoji humu ndani ya Baraza.

a) Hebu tueleze hiki chombo kishaahidiwa muda mrefu kuhusu *DNA* au imekuwa ni wimbo wa taifa hadi hii leo, tueleze lini chombo hiki kitapatikana ni muda mrefu wanachi walikuwa wakilalamika, lakini humu majibu yenyewe ni ya kisanaa hiki suala lenyewe hasa mkiliangalia kimsingi suala hamkulijibu lakini suala si langu na wala sikutaka kuliingilia.

b) Hebu tueleze hao wataalamu tayari wapo wa kushughulikia chombo hicho.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana nakushukuru Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

a) Kwanza kabisa nimshukuru na mimi kwa pongezi zake maana huwa hatuzipati mara kwa mara, lakini nashukuru kwa pongezi zake na kiliona jambo hilo kwamba hata tukiwa na udhaifu lakini kuna mema na mazuri mengi tunayafanya na mimi naomba nizifikishe pongezi hizo kwa madaktari wetu, madaktari bingwa pamoja na wauguzi wetu na *staffs* wote wa hospitali zetu zote wao ndio wanaostahiki pongezi hizo kwa kutoa mashirikiano, umoja wetu na upendo tuliokuwa nao. Kwa hivyo naomba nishukuru pamoja na wale waatalamu bingwa ambao wanakuja kututembele hapa kwa ajili ya kufanya operesheni hizo mbali mbali.

Mhe. Spika, bajeti ilitengwa mwaka huu kwa ajili ya mashine ya *DNA* na hivi sasa mchakato mzima wa tenda ushaanza, mashine hii ina gharimu zaidi ya bilioni moja. Kwa hivyo mchakato umeshaanza na kwa bahati mashine hii katika Afrika nzima kuna *agent* mmoja tu wa ku-*supply* mashine hii haziuzwi kila mahapa mashine hii.

Kwa hivyo kwa Afrika nzima kuna *agent* mmoja na jana nilikuwa nasoma ripoti bahati nzuri duniani kuna kampuni kama nne mpaka tano zinazotengeneza mashine ya aina hii. Lakini kwa Afrika yupo *distributor* mmoja na ofisi zao ziko Nairobi. Na kwa kupata uhakika nilishamtuma tayari Mkemia Mkuu kusafiri kwenda mpaka Nairobi kutafuta taarifa zote kwa sababu hatutaki mashine ije hapa halafu isifanye kazi baada ya miezi mitatu, tumeshatoa onyo hilo kwamba tunakachokinunua tunataka kidumu muda mrefu sana na ndio maana tumesema sasa hivi tuna kun haja ya kukutana na *distributor* mwenyewe kabla ya mchakato kwa sababu mmoja tu anaye-*supply*.

b) Mhe. Spika, pale panapopatikana vifaa wakati mwengine ama misaada inayokuja mikubwa, kwa kuwa kutokana na upungufu mkubwa wa bajeti, ndio maana unakuta kile kitu kinakuwepo pale kinasubiri mpaka bajeti ya kufunga ama ya kulijengea lile jenereta ama ya kutafuta ufundi wa kufunga. Kwa hivyo

mara nyingi inakuwa ni uhaba wa bajeti na tunapopata misaada hii huwa tunafuatilia kwa karibu sana kupata fedha husika ili tuweze kufanya kazi hiyo na zinapopatikana tu tunafanya kazi hiyo.

Naomba nishukuru sana kwamba fedha ya *DNA* hivi sasa tayari imeshatengwa na imeshapatikana tunasubiri michakato hiyo yote ikamilike ili tuweze kununua mashine hiyo, ahsante.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Afya kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza.

Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa nia njema ya kununua *DNA* ambalo ni jambo muhimu kwa nchi yetu na kutokana na mazingira tuliyokuwa nayo katika nchi yetu.

Lakini nimpe mfano tu Mhe. Waziri katuambia kwamba *DNA* hii katika Afrika itakuwa ndiyo ya mwanzo na ya mfano, lakini nataka nitowe tahadhari tu tulikuwa televisheni ya mwanzo Zanzibar katika Afrika, tumekuja mpaka tuka-*delay* tukapoteza malengo ya televisheni ile mpaka Mhe. Rais wa Zanzibar Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein akaifanyia *review* tena, yaani akaifanyia utaratibu tena wa kurudi katika hali yake ya zamani.(*Makofi*).

Suala langu liko hapa. Je, kwa kuwa chombo hili ni muhimu na chombo hiki cha gharama kubwa tuseme bilioni moja na zaidi kidogo. Hivyo Mhe. Waziri nimwambie kuna *CT Scan* katika hospitali yetu ukienda unambiwa mbovu au mtaalamu hayupo au ngoja kesho na kesho kutwa mtu anaathirika, atakuwa na utaratibu gani wa kuwaadhibiti hawa watendaji wa chombo hiki pindi kikifika ili ile kadhia ya mahitaji ya wananchi yajulikane yanapatikana bila ya matatizo.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Mhe. Ali Suleiman Ali kwa swali lake la nyongeza. Lakini namba kwanza kuna moja nililisahau katika suala lililopita la Mhe. Jaku Hashim Ayoub, nalo aliuliza wafanyakazi wangapi watakaoweza kutumia mashine hii ya *DNA*, mpaka jana tuna wafanyakazi watatu ambao wamesomea na watakaoweza kuiendesha ile mashine ya *DNA*, naomba hilo niliweke wazi; wawili wanawake, mmoja wakiume.

Sasa Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Ali Suleiman Ali utaratibu wa udhibiti. Sitaki kufungua yote sasa hivi hapa lakini tayari utaratibu wa udhibiti umeshaanza na vyombo husika vinafanya kazi na vimeshaanza kazi hiyo. Sasa sitaki kutolea ufafanuzi kwa sababu tunajiuliza masuala mengi, kwa nini mashine yetu kila mara iharibike za wenzetu hospitali za nje ziwe zinafanya kazi, hilo tunajiuliza.(*Makofi*).

Kwa nini lifti yetu igome kila mara ama iharibike kila mara, wakati lifti za wengine wote zinafanya kazi hayo yote tunajiuliza, tunajiuliza je, kuna kitu fulani ndani yake kuna *sabotage*. Kwa hivyo vyombo husika tayari vinafanya kazi mara tu watakapowasilisha ripoti yao sisi tutachukua hatua na Inshaallah hizo taarifa za hizo hatua tutawasilisha pia ndani ya Baraza la Wawakilishi, ili wananchi wote wapate kujua hatua zilizochukuliwa ahsante Mhe. Spika.(*Makofi*).

Mhe. Spika: Mheshimiwa kutokana na umuhimu wa swali hili nitawaongeza watu wawili nitaanza na Mhe. Hamad Abdalla Rashid na atafuatiwa na Mhe. Abdalla Maulid Diwani.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kuniona ndani ndani ya sehemu ya nyongeza na umuhimu wa swali lenyewe.

a) Mhe. Waziri pamoja na majibu mazuri uliyojibu katika Baraza la Wawakilishi, mimi ningependa kujua tu kwa sababu mashine nyingi za hospitali zetu zinaharibika kutokana na kupata ubaridi halisi unaohusika, vile vile mahali sahihi. Je, unatuthibitisha vipi mashine hii itakuwa salama kwa kupata ubaridi unaohusika na hata pengine ile *regulator* ya ku-*regulate* umeme ambao umesababisha shoti mara kwa mara kwa vyombo hivyo vya *eletronic*.

b) Kwa kuwa tayari utaratibu wa kununua mashine hii umeshafanyika Unguja, Wizara yako ina utaratibu gani kuhakikisha na Pemba kunafungwa mashine kama hii ili wananchi wa Pemba na wao wasisumbuke kuja Unguja.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Hamad Abdalla Rashid swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

a) Ni kweli anosema hayo yote lakini tunachojiuliza sisi baada ya kufanya marekebisho yote nitachukulia mfano huo huo wa *CT Scan*. Chumba chake tumefanya marekebisho ya umeme, tumetia nyaya mpya, tumetia *AC* mpya, tumetia *stabilizer* pale, lakini bado mashine inaharibika. Sasa mimi nilikwenda Dar es Salaam kutazama pia kwa wenzetu wanafanyeje na kutazama pia baada ile ziara ya Rais Magufuli aliyoifanya pale Hospitali ya Muhimbili. Jambo moja wenzetu waligundua kule na naomba hili nilitamke wazi bila ya kutafuna maneno, jambo moja walilogundua wenzetu kule madaktari wengi walikuwa wana hospitali zao binafsi ambazo wanazofanyia kazi. Sasa ili kupata wateja kule kwa sababu hizi mashine pia zipo katika hospitali binafsi na bei zake nyote mnazijua humu ndani, na nyote mnapeleka wagonjwa ili kupata wateja kule wa kutosha basi walitokezea baadhi ya mambo ambayo ndio hayo tunayafatilia sisi sasa hivi.

Sasa naomba niseme kwamba kwa upande wa umeme, upande wa *air condition*, upande wa hali na madhari ya vile vyumba husika ukipitia pale Hospitali ya Abdalla Mzee pale Mkoani utaona chumba chake ni kizuri kabisa, kisafi kipya, lakini mara unasikia hiki, mara unasikia hiki. Kwa hivyo hayo tunayafanyia kazi na naomba tuwachie vyombo husika vifanye kazi, kazi hiyo imeshakamilika tutajua wapi tunapochezewa, ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Spika, kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza, pamoja na pongenzi nyingi sana za Wizara ya Afya kupitia Rais wa Zanzibar kwa namna ambavyo wanavyopambana kuwa kwamba zitaletwa Hospitali ya Mnazi Mmoja inakidhi mahitaji ya Wazanzibari, tumeona ununuaji wa vifaa vyingi sana au mashine nyingi sana katika hospitali ile kwa ajili ya kuboresha afya.

a) Lakini hutokea na uharibifu wa kukosekana wataalamu wa mafundi (*technician)* wa ufundi katika mashine zile, tumegundua mashine *X-ray, CT Scan* na nyenginezo. Sasa hivi unakwenda kununua mashine ya *DNA* ni ya pesa nyingi. Je, kuna wataalamu wangapi pamoja ulosema kwamba una wataalamu ambao wanaweza kui-*monitor* ile kufanyia shughuli zake, ni wataalamu wangapi wa ufundi pindi kifaa kile kitakapokuja kuharibika.

b) Mashine hii ni ya pesa nyingi tunatumia zaidi ya *one point billion.* Je, tutapata *guarantee* ya muda gani ili isiionekane kwamba muda mdogo tu mashine imekuja hapa baada ya miezi mitatu mashine ile inaharibika *without guarantee*.(*Makofi*).

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Abdalla Maulid Diwani swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

a) Ni kweli kabisa kuna uchache wa hawa *Biomedical Engineers* wataalamu au mafundi sanifu wa vifaa vya tiba na upungufu huo sio hapa Zanzibar tu Tanzania nzima naweza kusema hata Afrika Mashiriki. Kwa hivyo hatua tuliochukuwa sasa hivi ni kuwasomesha vijana wawili ambao bado wako masomoni ili tuweze kupata mapema. Lakini pia tunawandeleza wale vijana ambao waliomaliza kozi pale Chuo cha Afya Mbweni kwa sababu kozi hii ilikuwa inatolewa Mbweni mpaka hivi karibuni. Kwa hivyo tunawandeleza wale vijana walioko pale Chuo cha Afya Mbweni.
Tumezungumza na wenzetu wa China katika timu yao inayokuja ya madaktari, safari hii tumeomba nafasi zile thelathini na mbili ambazo huwa tunazipata kutoka China madaktari wanakuja hapa basi tumesema bora tuondoshe daktari moja tuweke *engineer* mmoja. Tupate *engineer* katika timu ile ya wataalamu

wa Kichina wanaokuja ili mashine zetu ziweze kufanya kazi, kwa sababu madaktari tusipokuwa na mashine wale madaktari wanakuwa wamekaa wanafunga mikono kwa sababu hakuna mashine za kufanyia kazi za kuweza kutoa matokea. Kwa sababu daktari jambo la mwanzo anataka aidha *lab test* ama *imagine*, ama *radiology* yaani upigwe picha. Kwa hivyo tumeomba kupitia Ubalozi wa China na hiyo barua nimeandika mimi mwenyewe kuomba katika timu yao ya Wachina watakaokuja safari hii tunabadilisha kidogo mmoja awe *engineer* ili aweze kutusaidia.

Mhe. Spika, la pili ameuliza kwamba hii mashine ya *DNA* itakuwa na *guarantee* ya muda gani. Tulichofanya mpaka sasa hivi kuzungumza na hiyo kampuni ambayo makao makuu yake yako Nairobi, sisi tayari tumeshaanza mazungumzo kwamba kwa kuanzia tuwe na *guarantee* ya miaka miwili. Wao *standard guarantee* wanayotoa waki-*supply* mashine hiyo ni mwaka mmoja, sisi mpaka sasa tumeomba miaka miwli na bado tuna *negotiate* nao ili tuweze kuweka katika zile *tender terms and conditions*, masharti ya *tender* hiyo. Ahsante mheshimiwa.

Nam. 54

Mipango ya Kuandaa Timu ya Taifa Kiushindani

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza:

Katika sherehe za kuwapongeza vijana wa *Zanzibar Heroes*, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein alitaka Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kuondokana na tabia ya ushiriki katika michezo bali wawe washidani na kuachana na mizozo ambayo inapelekea kwenda Mahkamani badala ya maswala yao kumalizwa na vyama vyao vya michezo.

(a) Je, Wizara ina mpango gani kabambe ulioandaliwa kuhakikisha kwamba timu yetu itakuwa na ushidani mkubwa kutwaa taji kwenye mashindano yote yanayoandaliwa na *CECAFA*.

(b) Je kuna masharti gani wanayopewa klabu za Tanzania Bara ambazo zina wachezaji wa Taifa wanaochezea *Zanzibar Horoes* pindi wanapotakiwa kujerea au kuja kucheza timu yetu ya *Zanzibar Heroes*.

(c) Je kuna mikakati gani iliyopangwa kuhakikisha kesi zote zinazohusiana na mchezo wa mpira wa miguu haziendi Mahakamani na badala yake kesi hizo zimalizwe na *ZFA* wenyewe.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo - Alijibu:

Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza kabisa naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuamsha salama na kufika katika Baraza lako hili tukufu.

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 54 naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, ni kweli kuwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein aliitaka Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo itokane na tabia ya ushiriki katika michezo bali tuwe washindani katika michezo yote na kuachana na mizozo ambayo itapelekea kwenda Mahakamani badala ya masuala yao kumalizwa na vyama vyao vya michezo.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo mafupi sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam.54 lenye kipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo.

a) Mhe. Spika, wizara kwa kushirikiana na Idara ya Michezo itahakikisha kuwa Chama cha Mpira wa Miguu Zanzibar (*ZFA*) kinasimamia kufanyika maandalizi ya Timu ya Taifa mapema.

(b) Hakuna masharti yoyote waliyopewa vilabu vya Tanzania Bara ambavyo vina wachezaji wa taifa wanaochezea *Zanzibar Heroes*.

(c) Ili kuhakikisha kuwa kesi zote zinazohusiana na mchezo wa mpira wa miguu haziendi Mahakamni na badala yake kesi hizo zinamalizwa na *ZFA* wenyewe. Chama cha Mpira wa Miguu Zanzibar (*ZFA*) kimeeleza wazi katika Katiba yake kipengele Nam. 100(1)(i) na kwa kufuata maelekezo ya *FIFA* na *CAF*.Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza.

Kwa kuwa umesema hakuna masharti ni kweli hakuna masharti, lakini kuna utaratibu ambao unatumika kwa wachezaji wanaochezea vilabu pale zinapotokea timu zao za taifa kuchezea mashindano ya kimataifa.

a) Je, ni utaratibu gani nyinyi mnaotumia ambao itavitaka hivyo vilabu kwamba mara inapotokea wachezaji wetu wapo kwenye vilabu na timu yetu ya taifa inakabiliwa na mchezo ulioko mbele yao, na kwa sababu tunahitaji muda mrefu wa maandalizi kwamba vilabu hivyo vinawaruhusu wachezaji wale kujiunga na wenzao kwa wakati ili waweze kufanya mazoezi ya pamoja na kuiwezesha timu kupata ushindi.

b) Kwa kuwa ili timu ifanye vizuri inahitaji maandalizi ya muda mrefu kama nilivyoeleza na maandalizi ya muda mrefu yanahitaji fedha. Je, wizara ina fungu lolote ambalo inatenga kwa ajili ya kuisaidia timu ya taifa ambayo itakuwa na uwezo wa kukaa pamoja muda mrefu wakafanya mazoezi bila ya kupata ufadhili kutoka kwa wahisahi. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) yote kwa pamoja kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, utaratibu ambao tunautumia kwa vilabu vya wenzetu ambavyo wachezaji wetu wa timu ya taifa wako kule. Mhe. Spika nimjibu Mhe. Mwakilishi kwamba utaratibu huu upo ambapo wachezaji wetu pale tunapowataka wanahudhuria katika timu yetu ya taifa ya Zanzibar na kufanya mazoezi. Lakini tujue kwamba wachezaji wale wamechukuliwa na vilabu vile kama ni biashara. Kwa hivyo haipaswi na sisi kutunishiana misuli, hekma na busara inatakiwa itumike. Hivyo tunakuwa tunazungumza navyo vilabu hivi ili kuona wachezaji wetu wanashiriki katika timu yetu ya taifa ya *Zanzibar Heroes*.

Mhe. Spika, lakini kiko kifungu au bajeti ambacho tumetengewa kwa kuwasaidia timu zile za taifa wakati zinaposhiriki michezo ile ya kimataifa. Vile vile niwaombe sana Waheshimiwa Wawakilishi kifungu hiki pale wakati tunapoleta bajeti yetu kwa hiyo tunawaomba sana ili watupitishie na watuombee ziongezwe, ili ziwe nyingi kwa ajili ya wachezaji wetu ili wawekwe kambini mapema na watayarishwe mapema kwa ajili ya kushiriki timu ya taifa. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza lenye (a) na (b).

Mhe. Spika, kwanza nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake lakini mbali na majibu hayo naomba kuuliza swali hili.

Mhe. Spika, awamu ya sita iliyopita wakati ule Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo alikuwa Mhe. Ali Juma Shamuhuna ambaye pia akiwa Naibu Waziri Kiongozi na Naibu wake Waziri alikuwa Mhe. Mahamoud Thabit Kombo walifanya kazi kubwa katika kutafuta wafadhili kwa Timu ya Taifa ya *Zanzibar Heroes*, ligi kuu ya Zanzibar pamoja na mashindano ya *Mapinduzi Cup*. Kwa kweli niwape pongezi viongozi hawa kwa kazi kubwa waliyoifanya kipindi kile kwa kushirikiana na wadau mbali mbali kutafuta wafadhili katika kuendeleza mpira wetu wa Zanzibar.

a) Je, wizara ina mikakati gani ili kuhakikisha imewatafuta wafadhili wa kuifadhili timu yetu ya taifa au wadhamini wa Timu ya Taifa, ligi kuu ya Zanzibar na mashindano mengine makubwa kama yale *Mapinduzi Cup* ili kuondokana na omba omba wakati wa mashindano yanapofika.

b) Kwa kuwa Mheshimiwa amejibu kwamba kuna utaratibu wa hapa na pale katika timu yetu ya taifa wakati wachezaji wakenda kucheza nchi za nje. Lakini niseme tu kwamba siku zote inakukwa taifa kwanza, mchezaji yeyote anayecheza vilabu mbali mbali hata huko Ulaya huwa inapofika timu ya taifa inapocheza mchezaji yule hurusiwa kwenda kucheza timu yake ya taifa, ili kuhakikisha haya yanaondokana wachezaji kutokuchezea timu zao za taifa. Wizara inatoa tamko gani kwa vilabu hivi ambavyo havitoi ruhusa kwa wachezaji kuja kucheza timu ya Taifa.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza kabisa niendelee kumshukuru na kumpongeza sana Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo, kwa umahiri na ufatiliaji wake na kuweza kuwapa taarifa iliyokamilika Waheshimiwa Wawakilishi ndani ya chombo chako hiki tukufu.

Mhe. Spika, baada ya hayo naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi maswali yake mawili ya nyongeza kama ifuatavyo.

a) Mhe. Spika, ni kweli huko nyuma jitihada kubwa sana zimefanyika za kutafuta wafadhili kwa timu yetu ya taifa na vilabu mbali mbali. Jitihada hizo kwa awamu hii zinaendelezwa kama zilivyokuwa hivi, na mafanikio yalionekana wakati wa mashindano ya kombe la Mapinduzi, vile vile na timu yetu hii ya *Zanzibar Heroes* ambayo ilichukua ushindi mkubwa kabisa katika mashindano yake ya *CECAFA*.

Mhe. Spika, lakini mbali na jitihada hizo za kuwapata wafadhili ambapo kwa hivi sasa muelekeo unaonekana kuwa ni mzuri zaidi kuliko hata huko nyuma tunakotoka. Bado tuna mpango wa kuhakikisha kwamba vilabu vinawezeshwa na vinajiwezesha ili viweze kushiriki mashindano vikiwa na uwezo. Hatutaendelea kila siku kusubiri kuomba omba na kutafuta pahali ambapo panaweza kutufikisha pahali tusifanye michezo yetu ikawa ya kuvutia. Kubwa zaidi ni kuwa na mpango itakayoweza kuviwezesha vilabu na kuziwezesha timu zetu za taifa. Tuelewe tuna vyama 33 vya michezo na vyote hivyo vinahitaji ufadhili na sisi tunaweka mikakati kuhakikisha kwamba kuinuka kwa michezo basi ni kujiwezesha wao wenyewe.

(b) Ni kweli kwamba timu ya taifa ni muhimu kuliko vilabu kwa pale mchezaji anapotokea kuitwa kuchezea timu ya taifa. Hivyo, ndio inavyofanywa kwa timu za Tanzania Bara na timu zetu za Zanzibar, hapajatokea malalamiko yoyote, wala hapajatokea kukosekana kwa mchezaji yoyote wakati anapohitaji. Kuchelewa kunaweza kutokana na umuhimu wa mechi zinazoweza kujitokeza kwenye vilabu ambapo mchezaji yule anaonekana ana umuhimu wake. Hata hivyo, mashirikiano makubwa yanafanyika ili kuhakikisha mchezaji yule anawasili mapema inavyowezekana. Mashirikiano hayo yataendelea kuendelezwa iwe ndani ya Zanzibar na nje ya Zanzibar Mhe. Spika. Ahsante sana.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nakushukuru sana Mhe. Spika, na mimi nimshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri lakini nimuulize waziri kwamba tulipokwenda kwenye mashindano Kenya ya timu yetu ya *Zanzibar Heroes,* kuna timu ililalamika kwa kuona *speed* ya wachezaji wa Zanzibar ni kubwa wakaona wale labda wanatumia madawa. Lakini ile ilikuwa ni moja ya hoja ya kutupunguza nguvu ili tuweze kupata mambo ambayo hatutoweza kushinda.

a) Je, Waziri baada ya matokeo ameiandikia *CECAFA* barua gani ya kuilalamikia kesi ile ili mambo kama yale yasitokee tena.

b) Sasa hivi ndio tumeshapata funzo na tunaendelea katika mashindano yetu ya kimataifa. Je, Waziri wachezaji wake wote wa fani zote zinazokwenda nje katika mashindano wameshawapima watu hao au ambao wanawaandaa kwenye mashindano hayo.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Ahsante sana Mhe. Spika, napenda kujibu swali la Mhe. Mwakilishi lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Mhe. Spika, ni kweli kwamba kulitokea kutokuaminika kwa wacheazaji wetu lakini kutokuaminika kule kulitokana na mchezo mzuri ambao wameuonesha wachezaji wetu wa *Zanzibar Heroes*.

Baada ya kutokea yale wachezaji wetu baadhi walipimwa, ambao ni wachezaji wanne, kweli walipimwa na vipimo vilichukuliwa na *CECAFA* na vikapelekwa Afrika ya Kusini. Lakini uzuri uliokuwepo wale waliopima vipimo vile wenyewe walibaini kwamba ni vitu visivyo mashiko na namshukuru sana Balozi wetu wa Tanzania aliyeko nchini Kenya ambaye alikemea vikali suala lile lillofanyika kwa wachezaji wetu wa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla wake.(*Makofi*).

Mhe. Spika, barua tuliwaandikia na wao *CECAFA* walikiri kwa makosa waliyoyafanya, hususan makosa ambayo wameyafanya ghafla baada ya kuona kwamba tutaitoa timu yao ya Kenya.

b) Kuhusu wachezaji kuwapima wanapokwenda huko nje ya nchi, sisi hatuna mashaka kwa wachezaji wetu, Zanzibar vipaji vipo, Zanzibar mpira unachezwa, wachezaji wetu hawana haja ya kutumia madawa wala hawana haja ya kutumia nguvu za ziada kwenye miguu yao. Wachezaji wetu wana uwezo wa kila aina kuanzia ngazi ya chini miaka 15, miaka 20 na hata wanapokuwa wazee. Mfano, mzuri ni mchezaji Selembe ambaye amekuwa ana miaka 29 alikuwa mmoja katika mchezaji aliyepimwa na mchezaji aliyechukua ushindi wa kwanza kwa kukimbia masafa marefu ndani ya kiwanja, lakini kwa uhodari wake mchezaji yule na yeye bado amepata nafasi ya kwenda kuchezea nje na tayari ameondoka Zanzibar na kucheza nchi za nje. Kwa hivyo asiwe na wasi wasi hatuna haja ya kupeleka wachezaji wakenda wakapimwa, vijana wetu bado wataendelea kuchukua vipaji vyao ambavyo wamezaliwa navyo ndani ya taifa lao. (Makofi).

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri. Na swali moja la upendeleo Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis.

Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis: Ahsante nakushukuru Mhe. Spika, kwa kuniona na kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri na Mhe. Naibu Waziri ningeomba kuuliza swali la nyongeza lenye (a) na (b).

a) Mhe. Spika, kutokana na majibu mama ya Mhe. Naibu Waziri alieleza kuwa jibu (c) katika majibu yale alielezea kuhusu kesi zinazoenda Mahakamani na utaratibu uliokuwepo. Mhe. Waziri kuna kesi ngapi kwa sasa ambazo zipo Mahakamani na zinahusiana na nini.

b) Kwa kuwa Katiba ya ZFA ndio inayowaongoza kuna sababu gani kesi hizo zikapelekwa Mahakamani. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu swali lake Mhe. Mwakilishi lenye kipengele (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Mhe. Spika, kwa sasa hakuna kesi yoyote ambayo ipo Mahakamani.

b) Ni kweli kwamba tunaongozwa na Katiba na Kanuni za *ZFA*, yule ambaye kwa wakati ule alikwenda Mahakamani, alikwenda kwa utashi wake tu na kesi hii ndio maana Mhe. Hakimu akaiondosha ili zimalizwe katika kitengo

kile cha *ZFA* kama Katiba na Sheria ya *FIFA* inavyoelekeza. Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Spika: Mhe. Miraji Khamis Mussa ngoja nikupe upendeleo pia, haya endelea.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya upendeleo kuuliza swali la msingi katika *ZFA* yetu. Nilikuwa napata shida kidogo ninaposikiliza majibu ya Mhe. Naibu Waziri na Waziri mwenyewe kwa sababu sijui hata wanatumia Katiba ipi katika zile Katiba tatu za *ZFA*.

a) Lakini niwapongeze sana pamoja na maelezo hayo wamejibu vizuri, lakini hapa *ZFA* hivi karibuni katika kuendeleza michezo kulikuwa kuna uvumi wa maelekezokutoka *ZFA* kwa viongozi wa vilabu wa madaraja mawili. Daraja la ligi kuu na ligi daraja la kwanza kanda kuwa wataziteremsha timu sita Unguja na timu sita Pemba, kwa jumla yake kumi na mbili, kwa madaraja hayo mawili maana yake timu ishirini na nne zitashuka. Nilitaka kujua kauli hii na uvumi huu ni kweli au si kweli.

b) Kama ni kweli utaratibu gani utakaotumika katika Katiba hiyo ya *ZFA* kuzishusha timu hizi kumi na mbili, kwa maana ya sita Unguja na sita Pemba katika madaraja mawili kwa maana timu ishirini na nne zitashuka. Ahsante nakushukuru Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Ahsante naomba Waziri mwenyewe naomba utusaidie.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii na Michezo: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na kwamba sina wasi wasi kwamba Mhe. Naibu Waziri anaweza kulijibu hili suala kwa vizuri kabisa.

Lakini kwa faida ya Waheshimiwa wako wa Baraza la Wawakilishi Baraza lako tukufu na kwa kujibu suala la Mhe. Miraji Khamis Kwaza naomba kumjibu maswali yake mawili kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, ni kweli utaratibu tuliojiwekea wa kuzishusha timu kama alivyoueleza ndivyo utakavyotekelezwa na Mheshimiwa asiwe na wasi wasi kwa timu yake, timu yake naiamini ina uwezo, ina nguvu haitakuwemo katika zile sita zitakazoshushwa. Wakati Mhe. Miraji Khamis Kwaza yeye ni Rais wa timu yake, basi mauomba aongeze nguvu na jitihada na kuweza kuifadhili kama nilivyosema vilabu vyetu vinatakiwa kuwezeshwa ili kutandika *football* ndani ya visiwa hivi.

Lakini utaratibu huo utakaotumika Mhe. Spika, utaondoa utaratibu uliokuwepo wa sasa hivi wa kuwa na timu nyingi zisizoendana na idadi ya watu ndani ya visiwa vyetu. Kwa mujibu wa Katiba yetu ya *ZFA* na Katiba ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Barani Afrika (*CAF)* na Katiba ya *FIFA* zote kwa pamoja zina maelekezo ya kuwa na vilabu maalum kutokana na idadi ya watu waliokuwepo ndani ya nchi ile.(*Makofi*).

Kutokana na hiyo makosa tuliyoyafanya huko nyuma ya kuwa na timu 14 Pemba na 14 Unguja na kuwa na idadi ya vilabu vingi ndani ya *premier* kuliko nchi yoyote duniani ni lazima tuziteremshe timu hizo, ili tuende sambamba na mfumo uliokuwepo katika michezo huu wa mpira wa miguu. Kwa hiyo, timu tutazipandisha 2, tutateremsha timu 12 na tutabatikiwa na timu 16 ambazo hazitabagua Unguja wala hazitabagua Pemba.

(b) Hii itazipa motisha timu za daraja la kwanza kuweza kurejesha hadhi ya mpira uliokuwepo zamani katika kungangania kuingia ligi ya *premier*. Ligi ya *premier* itakuwa ni finyu ili uingie mle uhodari unawezekana ukawa ni mkubwa sana. Kwa hivyo, Mheshimiwa aweze kulinda tu lile daraja la kwanza asiteremeke daraja la pili. Ahsante sana Mhe. Spika. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsanteni Waheshimiwa wakati wa maswali umekwisha na Mhe. Jaku Hashim Ayoub nimekuona. Kuhusu utaratibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub halafu nitapata muongozo kutoka kwa Mhe. Mohamed Said Mohamed.

Utaratibu

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Spika, kwanza nikushukuru sana na nikupongeze kabisa. Nimesimama kanuni ya 42, sijui niisome Mheshimiwa au umeshakuwa na uzoefu nayo.

Mhe. Spika, kuna msemo unaosema, "Anayehangaika hachoki akishakupata utamuona". Mimi nina kilio changu kile kile na leo Waziri wa Afya kanipa matumaini mazuri sana nimemuona yuko juu ya fomu kwa kusema ukweli leo. Maana yake ule munkari wake kidogo kapunguza leo hata alipokuwa akijibu maswali alikuwa anatumia hekma kabisa nimpongeze kwa hilo. (*Makofi*)

Mhe. Spika, Baraza hili limeahidiwa Kauli ya Serikali na Baraza kesho kutwa linakwisha Mwenyezi Mungu akitujaalia Jumatano. Hali bado tete Hospitali ya Mnazi Mmoja kuhusu *lift* na *lift* ile niliofanya uchunguzi karibu watu mia tatu au mia nne wanaopanda kwa siku na kuna mbili, mimi niliomba alau iwe moja kwa dharura itengenezwe au inunuliwe mpya, maana yake karibu mwaka na wanaoumia ni wanyonge wakulima na wavuvi wa nchi hii.

Sasa Kauli ya Serikali bado sijaipata. Kwa hiyo naomba tujadili jambo la dharura kwa kweli hali hairidhishi ukienda pale jioni ukikaa machozi yatakutoka Mhe. Spika, wananchi wanaumia. Kauli za Serikali bado sijaipata mpaka sasa hivi na *lift* yenyewe ni kati ya milioni mia moja na hamsini mpaka mia mbili na karibu mwaka na ushahidi huo ninao.

Sasa niiombe sana serikali nipate kauli kabla Baraza halijesha, vyenginevyo kama ni ripoti hiyo mpaka mwezi wa tisa tutapokuja, wananchi watazidi kuumia, ukienda jioni pale ajali zinazotokea wagonjwa wanavyobebwa machozi yatakutoka. Kwa hivyo naona muda unakwenda na Kauli ya Serikali bado sijaipata Mheshimiwa. Nikuombe sana kwa heshima kabisa tusaidiane hili suala si langu mimi wala si la watu wa Paje, kwa ujumla watu wa Unguja na Pemba linawahusu suala hili wakiwemo wananchi wa Kiembesamaki.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Jaku Hashim Ayoub Mhe. Waziri wa Afya bahati nzuri nimemuona na yeye ananyanyuka.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii na naomba pia nimshukuru Mhe. Mwakilishi ila Kanuni aliyoitaja 42 ukenda kwenye kifungu cha (4) na hili naona likitokezea katika wiki hii mara kadhaa kwa sababu Mhe. Jaku Hashim Ayoub alikuwa analizunguzia hili suala la *lift* mara kadhaa ambalo serikali inaendelea kulifanyia kazi, hiyo ndio kauli rasmi.

Isipokuwa katika 42(4) “Kadri inavyowezekana kabla ya kikao kuanza Mjumbe atakuwa amewasilisha kwa Spika kwa maandishi maelezo ya jambo atakalopenda au analopenda lijadiliwe”.

Sasa Mhe. Spika, hili niliwahi mimi kuuliza kupitia meza ya Katibu kwamba hizi kauli zinatolewa ghafla zinarembewa rembewa. Lakini je, kuna chochote kilichowasilishwa mbele ya meza ili tukichukuwe kile sisi kama serikali, tukichukuwe kile kilichowasilishwa tukakifanyie kazi halafu tutoe kauli rasmi ya serikali.

Mhe. Spika, ningeomba mimi muongozo wako kwa 42(4) Je, hili limewasilishwa mezani ikiwasilisha hata mimi nakuwa na nguvu zaidi. Ahsante Mhe. Spika. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante Mheshimiwa nadhani kama utakuwa umemsikiliza vizuri Mhe. Jaku Hashim Ayoub amewali kulizungumzia suala hili nafikiri mmewahi kulitolea maelezo, hata leo nafikiri umeligusia kidogo na mimi sitaki niruhusu mjadala wa suala hili hapa sasa hivi, anachokikumbushia ni kwamba serakali iliahidi maana yake mlisimama mkaahidi kwamba mtakuja kulitolea maelezo.

Sasa hayo maelezo ndio Mhe. Jaku Hashim Ayoub alikuwa anayakumbushia tu sio kwamba tuwe na mjadala hapa. (*Makofi*).

Baada ya hapo naomba sasa nimwite Mhe. Mohamed Said Mohamed.

MUONGOZO

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Spika nikushukuru sana kwa kuniona lakini kubwa leo nilikuwa naomba muongozo wako.

Mhe. Spika, juzi kwenye mazungumzo baada ya bahari ya *ZBC radio* lilisemwa Baraza lako Tukufu. Mhe. Spika, lilizungumzwa kuwa Baraza lako Tukufu linakuwa na kauli mbaya zisizostahiki kwenye Baraza hili na jambo hili limeleta taswira mbaya sana mbele ya jamii kuwa sisi viongozi wa wako wa Baraza lako tunazungumza kauli zisizo za hakika.

Mhe. Spika, Baraza ni muhimili kama muhimili wa serikali, kama muhimili wa Mahakama na Baraza lako sio Idara ya Serikali. Jambo hili limezungumzwa linatuletea tofauti ndani ya jamii. Sasa nilikuwa nataka kujua Baraza lako Tukufu limeweza kuchukuwa hatua gani au serikali imechukuwa hatua gani kwa sababu Wajumbe wako sisi tuna kinga na fursa tukisema katika Baraza hili.

Mhe. Spika, naomba tu muongozo wako. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Mohamed Said Mohamed kwa muongozo ambao unauomba. Waheshimiwa Wajumbe labda tukumbushane tu kwa mujibu wa Kanuni na kwa mujibu wa Sheria ya Kinga ya Baraza la Wawakilishi, tuna haki ya kuzungumza ndani ya Baraza la Wawakilishi jambo lolote tu. Lakini tunachopaswa kufanya ni kutumia lugha za staha, tusitoe lugha ambazo ni za matusi wala tusiwatuhuwa watu kwa majina ambao hawawezi kuja kujitetea humu ndani ya Baraza la Wawakilishi.(*Makofi*).

Sasa hivyo hivyo, watu wa nje au vyombo vyengine au taasisi nyingine, Jumuiya yoyote kule nje isimuhukumu Mheshimiwa kwa jambo lolote analolizungumza humu ndani kwa sababu tuna kinga ya kisheria kwa chochote tunachokizungumza humu, hatuwezi hata kushitakiwa Mahakamani kwa ulilolisema humu. Kama kuna mtu anahisi kakwaza na chochote ambacho kimezungumzwa ndani ya Baraza la Wawakilishi, basi wajibu wake ni kumuandikia Spika lile lalamiko, halafu sisi tuna Kamati yetu ya Maadili tutaipelelekea lile lalamiko watalifanyia kazi wataangalia na *hansard* na tarehe

ya lile tamko lililotoka ambalo halikumridhisha mtu au taasisi na baada ya hapo huwa linatolewa uamuzi humu ndani ya Baraza la Wawakilishi.

Kwa hivyo nafikiri sote tukiwa tunazisimamia Sheria na Kanuni zetu, tutakuwa tuko salama tu, kama hichi ni chombo cha serikali kilichofanya hivyo bahati nzuri Mhe. Waziri yupo wanaweza wakenda wakatizama huko, kwa sababu mimi sijaona wala sijasikia na hili ndio limetolewa hapa ili tujuwe tunaendeleaje baada ya hapo.

Waheshimiwa nashukuru sana na baada ya hapo nakuona Mhe. Hamza Hassan Juma nakuona na wewe sasa.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, kwanza nakushukuru kwa kuweza kutoa ufafanuzi mzuri lakini vile vile kuweza kulinda heshima ya chombo hichi cha Baraza la Wawakilishi.

Suala langu kama alivyosema Mhe. Mohamed Said Mohamed kwamba kwa kuwa tayari kuna taasisi zinaanza kuingilia muhimili wa Baraza la Wawakilishi. Sasa na wewe unasema bado hujapokea taarifa yoyote ya kutaka labda kuchunguzwa au kuchukuliwa hatua jambo hilo.

Sasa Mhe. Spika, sasa suala hili kama mfano itakuwa imegundulikana kwamba kuna taasisi yoyote aidha ya serikali au jumuiya au yoyote imekwenda kinyume na Kanuni zetu na Sheria na Kinga na Fursa ya Baraza. Je, kuna hatua mahususi ambayo itaweza kuchukuliwa lakini vile vile kama itaonekana kweli labda kuna barua au kuna hoja ambayo imekuja kwako kama kuna Mjumbe ambaye amekwenda kinyume cha taatibu za sheria.

Je, ni chombo gani ambacho wewe unakiongoza na unakisimamia kitakachoweza kukichukulia hatua stahiki za kisheria.

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Hamza Hassan Juma labda nikusaidie na wewe kwa kuendeleza ule ule muongozo wa Mhe. Mohamed Said Mohamed ambao ameutoa ni kwamba ndani ya Baraza la Wawakilishi bahati nzuri tunayo Kamati ya Maadili. Kamati hii linapotokezea tatizo lolote la namna hii na hili jambo likaweza kumfika Spika rasmi basi huwa tunaliwasilisha kwenye hiyo kamati na hiyo kamati itakwenda kulifanyia kazi kwa kuangalia *hansard*, ili kama kuna chochote ambacho Mjumbe amekisema au kama ni mtu wa mje inaweza ika-*summon* akaja kwenye kamati halafu akatoa maelezo kuhusiana na Kanuni ya chombo hichi. (*Makofi*)

Baada ya kufanya kazi hiyo kamati hiyo ile ripoti yake inaileta humu ndani ya Baraza la Wawakilishi, halafu ndio hatua zinachukuliwa ndani ya hapo. Mimi

nadhani tufateni tu utaratibu kama kuna jambo lolote kauli za Waheshimiwa ambazo zinatoka ambazo zinawakwaza hapa hata waananchi huko nje, kama moja kwa moja atakuwa ameshutumiwa mtu basi mtu aje alalamike kwa Spika na kamati hii nitahakikisha inafanyakazi. Ahsanteni sana Waheshimiwa.

Mhe. Mwanaasha Khamsi Juma naomba uje uchukuwe kiti halafu tuendelee.

Samahani kulikuwa na matangazo ya wageni nilikuwa nimeshahau ngoja kidogo nimalizie wageni. Wageni ni wa Mhe. Rashid Ali Juma Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo ambaye pia ni Mwakilishi wa Jimbo la Amani, hawa ni wana *SACCOS* wa kikundi cha "Hatubagu cha Mtofaani", jumla yao ni 16 wanaongozwa na ndugu Lila Mrisho Mtwana ambaye ni Makamu Mwenyekiti, naomba asimame, Ndg. Merry Machel Sakoma Katibu, Ndg. Subira Mlekwa ambaye ni Mshika Fedha. Mnaona wapo wengi hapo ambao hawajatajwa lakini ningekuombeni nyote msimame *SACCOS* nzima ili muionekane mlivyopendeza. Ahsanteni sana na karibu sana Baraza la Wawakilishi na hongera sana Mhe. Rashid Ali Juma maana wapendeza sana. (*Makofi*)

SACCOS hii hatubagui ina wanachama wapatao 53 na leo wamekuja kutizama shughuli za Baraza na baadae kuonana na viongozi wa Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Wanawake, Wazee, Vijana, Watoto pamoja na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa lengo la kuimarisha kikundi cha wanaushirika. Karibuni sana Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma karibu sana. (*Makofi*)

(Hapa Mhe. Mwenyekiti Mwanaasha Khamis Juma alikalia kiti)

HOJA ZA KAMATI

Ripoti ya Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo ya mwaka 2017-18

Mhe Rashid Makame Shamsi (Mhe. Mwenyekiti wa Kamati na Sheria ndogo ndogo): (Ahsante sana Mhe. Mwenyeiti, kwa kuweza na mimi kuniruhusu kuweza kutoa ripoti hii ya Kamati ya Kanuni na Sheria ndogo ndogo ya kudumu ya Baraza.
Mhe. Mwenyekiti, naanza kuwasilisha hotuba hii kwa Kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutuwezesha leo kukutana tena katika ukumbi huu wa Baraza la Wawakilishi kutekeleza majukumu yetu ya kikatiba na ya sheria ya kuwawakilisha wananchi wetu kupitia chombo chao hiki muhimu. Ni

matumaini yangu kuwa kazi tunayofanya hapa inaleta manufaa makubwa kwa wananchi na taifa kwa ujumla.

Mhe. Mwenyeiti, pia nianze kutanguliza shukurani zangu binafsi kwako wewe na uongozi wa Baraza la Wawakilishi kwa kazi kubwa na masharikiano mliyoipatia Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo katika kipindi hiki kifupi hata tukaweza kuwasilisha ripoti yetu hii kwa mara ya kwanza kabisa. Tunatambuwa kuwa Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo kwa muda mrefu imekuwa kwenye Kanuni zetu lakini haikupata kuundwa na kufanya kazi zake kwa nyakati zote hizo.

Mhe. Mwenyeiti, chini ya Uongozi wa Spika wa Baraza hili Kamati hii imeundwa rasmi na kupangiwa kazi za kufanya kwa mujibu wa Kanuni ya 106 ya Kanuni ya kudumu za Baraza la Wawakilishi Toleo la mwaka 2016 ambayo imeainisha majukumu ya Kamati ya Kanuni na sheria Ndogo Ndogo kwenye jadweli la kwanza la Kanuni hizo, ambapo majukumu yake ya msingi ni kama yafuatayo:-

a) Kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa kwenye ripoti ya Kamati ya mwaka uliotangulia;
b) Kuchambua Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo ili kujiridhisha iwapo zimekidhi matakwa ya masharti ya Katiba, Sheria mama, na Sheria nyengine za nchi hii;
c) Kujadili na kutoa mapendekezo kwa taasisi husika juu ya namna bora ya kutengeneza Kanuni na sheria ndogo ndogo;
d) Kulishauri Baraza kupitisha azimio la kubatilisha Kanuni au sheria ndogo ndogo ambazo zinakiuka masharti ya Katiba, masharti ya Sheria Mama, au sheria nyenginezo za nchi;
e) Kufikiria jambo jengine lolote litakalopelekwa na Spika.

Mhe. Mwenyeiti, katika kipindi hiki kifupi Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo imefanyakazi zake za utekelezaji wa majukumu hayo ya Kikanuni kwa mashirikiano makubwa na Taasisi mbali mbali za wizara tatu ambazo Kanuni zake zimepitiwa na Kamati. Wizara zenyewe ni Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko.

Mhe. Mwenyeiti, Kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo nawapongeza sana kwa dhati Mawaziri wa Wizara hizo na Makatibu wao Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu, Wakurugenzi, Wakuu wa Taasisi, Vitengo na Watendaji wa kada mbali mbali za wizara hizo kwa mashirikiano yao hayo kwa Kamati yetu ambayo Mhe.Mwenyekiti**,** Kamati ya

Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo inawasilisha ripoti yake kutokana na shughuli mbali mbali ilizofanya katika kipindi cha mwaka 2017/2018 ambapo wajumbe wa Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo walifanyakazi kwa kiasi kikubwa na kwa mashirikiano kwa muda huo mfupi hadi kufanikisha kuwasilisha ripoti yetu ya awali kwa mujibu wa kazi zilizofanyika. Naomba nichukuwe fursa hii kuwashukuru sana wajumbe wa Kamati na kwa kutambuwa na kuthamini mchango wao naomba niwataje kwa majina kama ifuatavyo:-

1.	Mhe. Rashid Makame Shamsi	Mwenyekiti
2.	Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	Makamu Mwenyekiti
3.	Mhe. Mohammed Said Mohammed	Mjumbe
4.	Mhe. Ame Haji Ali	Mjumbe
5.	Mhe. Shaibu Said Ali	Mjumbe
6.	Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Mjumbe
7.	Mhe. Zulfa Mmaka Omar	Mjumbe

Mhe.Mwenyekiti**,** shughuli za Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo kwa kipindi chote hicho zimekuwa zikiratibiwa na Makatibu wawili kutoka Ofisi ya Baraza la Wawakilishi, ambao wametoa mashirikiano makubwa kwa Kamati na wametusaidia kwa ushauri wa mambo mbali mbali ikiwemo sheria, naomba niwataje majina yao kama ifuatavyo:-

1. Ndugu Khamis Hamad Haji; na
2. Ndugu Haji Jecha Salim

Mhe.Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo naomba sasa nijielekeze kutoa muhutasari wa kilichomo katika ripoti ya Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo kwa mwaka 2017/18 baada ya shughuli mbali mbali zilizofanywa na Kamati hii katika kipindi hicho.

Mhe.Mwenyekiti**,** utakumbuka kwamba kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo iliteuwa wajumbe wake mnamo tarehe 23/06/2016 huku kukiwa na maelekezo kuwa Kamati ikutane haraka kuchagua viongozi wake na kupanga utaratibu wa kazi zake. Mnamo tarehe 24/06/2016 Kamati ilikutana na kuchaguwa Mwenyekiti wake na Makamo Mwenyekiti ambaye ndie wewe kama nilivyotangulia kuwataja kabla. Nichukue fursa hii Mhe. Mwenyekiti kwa kuwashukuru kuwapongeza na wajumbe wa kamati yangu kwa kunichagua mimi kuwa mwenyekiti na kukuchaguwa wewe kuwa Makomo Mwenyekiti.

Mhe.Mwenyekiti, napenda ifahamike kuwa haikuwa rahisi kwa Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo kuanza kazi zake kwa vile Kamati hii ndiyo kwa mara ya kwanza imeundwa; na Wajumbe wake wote ni wapya ambao hao vile vile ni wajumbe kutoka Kamati nyengine mbali mbali za kudumu za Baraza la Wawakilishi. Hivyo kutokana na hali hiyo hatua ya kwanza kabisa ilikuwa ni kuipatia mafunzo Kamati hii ili ifahamu kwa kina majukumu yake na namna inavyotakiwa kufanya kazi zake. Mpango wa Mafunzo uliratibiwa vizuri na Ofisi ya Baraza la Wawakilishi, na Kamati ikapata mafunzo kwa awamu mbili.

Mhe.Mwenyekiti, awamu ya kwanza ya mafunzo ilianza mnamo mwezi wa Agosti, 2016 ambapo Kamati ilipata mafunzo kuhusu Sheria, Kanuni na uzoefu wa mabunge mengine yenye Kamati za aina hii ambazo husimamia utungaji wa Sheria Ndogo Ndogo na kanunuzi zake. Mafunzo hayo yalifanyika kwa mafanikio makubwa na wajumbe wa Kamati waliweza kufahamu kwa undani kuhusu Kanuni zinazotungwa kutokana na Sheria na namna Kamati nyengine za Sheria ndogo ndogo za Mabunge ya Jumuiya ya Madola zinavyofanyakazi zakekwa kupitia Kanuni hizo.

Mhe.Mwenyekiti, awamu ya pili ya mafunzo ya Kamati ilifanyika mnamo mwezi wa Agosti, 2017; Mhe. Mwenyekiti katika awamu hii ilihusisha mafunzo ya kuzitambuwa, kuzipitia na jinsi ya kuchambua sheria ndogo ndogo pamoja na uzoefu na utendaji wa Kamati ya Sheria Ndogo Ndogo ya Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kamati pia ilifanyakazi kwa vitendo ya kuchambua Kanuni ya Utalii ya Zanzibar ikiwa ni sehemu ya mafunzo yake ya vitendo.

Mhe.Mwenyekiti, Baada ya mafunzo hayo Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo ilifanya tathmini na kuandaa ripoti ambayo ilikabidhiwa kwa Ofisi ya Katibu wa Baraza la Wawakilishi na nakala yake kutumwa kwa Mheshimiwa Spika, ikiwa na mapendekezo mbali mbali ya namna ya kuiwezesha Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo kufanya kazi zake kwa ufanisi.

Mhe.Mwenyekiti, Hata hivyo, mpaka tunaripoti kwenye Mkutano huu Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo haikuwahi kupata mrejesho wowote wa mapendekezo hayo kutoka Ofisi ya Baraza la Wawakilishi wala Ofisi ya Mheshimiwa Spika.Lakini ni matumaini yetu kuwa mapendekezo hayo yatafanyiwa kazi ipasavyo kwa utulivu; na kama yatapata mwitiko na mrejesho ulio chanya basi ni imani ya Kamati yatasaidia sana Kamati hii kufanyakazi zake kwa uweledi mkubwa na kupunguza baadhi ya vikwazo vya Kikanuni vinavyoikabili Kamati kama nitakavyofafanua huko mbele.

SHUGHULI ZA KAMATI KWA MWAKA 2017/2018

Mhe.Mwenyekiti, Kamati ya kanuni na Sheria Ndogo Ndogo iliendelea na kazi zake za kupitia Kanuni za Sheria zilizoletwa na Serikali katika Mkutano wa nane wa Baraza la wa Wawakilishi. Kanuni hizo ni Kanuni za Huduma za Serikali za Mitaa za mwaka 2017 zilizotungwa na Waziri kutokana na Sheria ya Serikali za Mitaa namba 7 ya mwaka 2014 na kusainiwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za *SMZ*, Kanuni ya pili ilikuwa ni Kanuni ya Mirathi ya Kiislamu za mwaka 2016 zilizotungwa chini ya Sheria ya Kamisheni ya Wakf na Mali ya Amana, sheria namba 2 ya mwaka 2007, ambazo zimesainiwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Kanuni ya tatu ambayo kamati imeipitia ni Kanuni ya Makampuni ya Sheria Namba 15 ya mwaka 2013 ambayo matokeo ya uchambuzi wake hivi sasa yamo katika hatua za uchapaji.

Mhe.Mwenyekiti, sambamba na kazi ya kupitia Kanuni hizo, Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo kwanza ilifanya ziara ya kutembelea Taasisi mbali mbali za Serikali zinazohusika katika Utungaji wa Sheria na Kanuni, pamoja na baadhi ya Taasisi ambazo Kanuni zao zimepitiwa na Kamati. Katika ziara hizo Kamati imejifunza mambo mengi yanayohusu taratibu za kutunga sheria na kanuni na namna nzuri ya kutunga sheria na kanuni ambazo hazitaleta athari kwa wananchi ambao ndio watumiaji wakubwa wa sheria na Kanuni hizo. Mambo hayo yote yameelezwa kwa kirefu kabisa katika ripoti ya kamati iliyowasilishwa wajumbe.

MAMBO YALIYOBAINIKA WAKATI WA UTENDAJI KAZI WA KAMATI

A. ZIARA YA KAMATI KWA TAASISI ZA UTENGENEZAJI WA SHERIA

Mhe.Mwenyekiti, Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo ilifanya ziara ya kutembelea Taasisi mbali mbali za Serikali zinazohusika na utengenezaji wa Sheria na Kanuni kama nilivyoeleza hapo awali kwa nia ya kujifunza na kujiongezea ufahamu wa namna bora ya Kanuni na Sheria ndogo ndogo zinavyotengenezwa. Baadhi ya Taasisi hizo muhimu kamati zilizotembelea ni hizi zifuatazo:-

i. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

Mhe.Mwenyekiti, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inahusika kwa kiasi kikubwa katika kutengeneza Sheria na Kanuni za nchi yetu. Kamati ilikutana na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu na watendaji wake wakuu katika Uandishi wa Sheria na Kanuni. Mambo mbali mbali muhimu tumejifunza kupitia

majadiliano na hatimaye kushauriana juu ya hatua mbali mbali za kufanya katika kuhakikisha Kanuni zinazotungwa zinakuwa bora zaidi na zinazotekelezeka. Mhe. Mwenyekiti nichukue fursa hii kwa kumshukuru kwa dhati kabisa Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu na watendaji wake wote kwa kutupokea na kutueleweshа vya kutosha vya kutosha kuhusu utungaji wa Kanuni na hasa ushauri wao wa kutaka kuwepo kwa ushirikishwaji wa kutosha wa Wanasheria wa Mawizara na Taasisi nyengine za Serikali suala zima la utungaji wa Kanuni za sheria ndogo ndogo za hapa Zanzibar.

ii. Wakala wa Serikali wa Uchapaji

Mhe.Mwenyekiti, Kamati yetu tumepata pia fursa ya kukutana na Watendaji wa Wakala wa Seriali wa Uchapaji ambao wanahusika moja kwa moja nauchapishaji wa machapisho mbali mbali ya Serikali zikiwemo Sheria na Kanuni. Tunawapongeza sana kwa kutuelimisha mengi; na kubwa zaidi wametaka mashirikiano baina yao na Taasisi za Serikali zinazopeleka kazi zao kwa ajili ya kuchapishwa hususan Sheria na Kanuni. Mhe. Mwenyekiti nichukue fursa hii ya kuumpongeza sana Mkurugenzi wa Wakala na watendaji wake kwa mashirikiano yao.

iii. Tume ya Kurekebisha Sheria

Mhe.Mwenyekiti**,** Tume ya Kurekebisha Sheria ni moja ya vyombo muhimu sana katika hatua za utungaji wa Sheria za nchi na Kanuni zake. Kamati imepata nafasi ya Kukutana na Mwenyekiti wa Tume na Watendaji wake wakuu ambao walitupa mashirikiano mkubwa kwa kutufahamisha hatua mbali mbali za mapitio ya Sheria na hatimaye Kanuni. Jambo kubwa na zuri zaidi ambalo Tume ya Kurekebisha Sheria inafanya katika mchakato wa Kupitia Sheria hii ni Ushirikishwaji wa Wananchi katika hatua mbali mbali na hatua za awali kabisa za mapitio ya Sheria.

Mhe.Mwenyekiti Kamati yangu imejifunza vya kutosha umuhimu wa kuwashirikisha wananchi katika hatua za awali za kutengeneza Sheria, kwa kuwa wao ndiyo walengwa wa moja kwa moja wa matumizi ya Sheria hizo. Kamati yangu imejifunza zaidi kuwa kwa vile kuna umuhimu wa kuwashirikisha wananchi katika hatua za Kutunga sheria, ni muhimu zaidi pia kuwashirikisha katika hatua za awali za utungaji wa Kanuni ambazo zinafafanua utekelezaji bora wa sheria hizo.

Mhe.Mwenyekiti ,Tumepokea ushauri wa Tume ya Kurekebisha Sheria ya kutaka kuongezwa na kuimarishwa zaidi kwa mashirikiano na Taasisi nyengine za Serikali katika hatua mbali mbali za kutengeneza Sheria na Kanuni. Jambo hili ni muhimu ukizingatia kuwa Tume ya Kurekebisha Sheria inafanya utafiti

na kwenda mbali zaidi kwa wananchi wa kawaida kujuwa mahitaji ya Sheria yaweje na mwitikio au utekelezaji wa Sheria utakuwaje. Kamati inatoa wito kwa Taasisi za Serikali kuzingatia ushauri huu kwa kuongeza zaidi mashirikiano na Tume ya Kurekebisha Sheria ili sheria na Kanuni zinazotungwa ziwe na manufaa zaidi kwa wananchi wetu.

UTARATIBU WA KAMATI KUPITIA KANUNI NA SHERIA NDOGO NDOGO

Mhe.Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kusema hapo juu wakati nikiainisha majukumu ya Kikanuni ya Kamati hii, kazi kubwa ya Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo ni kupitia na kuchambua Kanuni na kujiridhisha kama Kanuni zilizotungwa hazipingani na Katiba, Sheria mama, Kanuni nyengine na sheria nyenginezo za nchi.

Mhe.Mwenyekiti, utaratibu wa Kamati kupitia na kuchambuwa Kanuni hadi kuweza kubaini mambo hayo siyo kazi nyepesi hata kidogo, kwanza Kamati inalazimika kuipitia kwa kina sana Sheria mama na pengine sheria mbali mbali zinazolinga na maudhuwi ya Kanuni husika, lakini pamoja hilo kamati inaangalia baadhi ya vipengele vya katiba kama vinahusika na baadhi ya masharti ili kujiridhisha kama vipengele hivyo havijavunjwa na Kanuni husika.

Mhe.Mwenyekiti, Kamati ya Kanuni na Sheri na Ndogo Ndogo pamoja na hilo pia hulazimika kuchambua sheria hiyo kwa lengo la kuweza kubaini maeneo mbali mbali ambayo sheria imekasimu kwa mamlaka kwa Waziri au chombo kinachohusika na sheria kwa kuyatungia Kanuni.

Mhe.Mwenyekiti, Kamati baada ya kuyabaini maeneo hayo yaliyopaswa kutungiwa Kanuni hapo ndio huanza kuchambua kwa undani na kwa umakini Kanuni husika. Kazi hii Mheshimiwa Mwenyekiti, huhitaji muda wa kutosha, huhitaji utulivu mkubwa lakini maarifa mengi hadi kukamilisha kazi hio, na hapa ndio uchunguzi hubaini ubora na mapungufu yaliyojitokeza katika Kanuni hiyo.

Mhe.Mwenyekiti, Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo pia hulazimika kuchambua sheria hiyo kwa lengo la kubaini maeneo mbali mbali ambayo sheria imekasimu.

Mhe.Mwenyekiti**,** Katika mchakato wa kazi hii Kamati inapaswa kukutana na makundi ya watu tofauti yanayohusika na matumizi ya Kanuni hizo wakiwemo watunzi, wasimamizi pamoja na wananchi ambao ndio walengwa na watumiaji wa Kanuni husika na kujadiliana nao juu ya namna walivyoshirikishwa katika Utengenezaji wa Kanuni hizo na maoni yao kwa ujumla kuhusu matumizi ya

Kanuni hizo. Kamati inafanya hivyo kwa lengo la kutekeleza ule wajibu wa Kikanuni wa kutakiwa kutoa mapendekezo kwa Serikali kuhusu namna bora ya utungaji wa Kanuni na Sheria ndogo ndogo.

Mhe.Mwenyekiti**,** Kamati pia, inapata nafasi ya kukutana na Waziri anayehusika na utungaji wa Kanuni hiyo pamoja na Watendaji wake ambapo yale mambo ya msingi ambayo Kamati imejadiliana na wahusika mbali mbali inajadiliana na Wizara pamoja na kubaini yale maeneo yenye mapungufu yaliyojitokeza.

B. MATOKEO YA UCHAMBUZI WA KANUNI ZA HUDUMA ZA MAMLAKA YA SERIKALI ZA MITAA

Mhe.Mwenyekiti**,** Kanuni hii ni ya mwanzo kufanyiwa kazi na Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo. Kanuni ya Huduma ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2017 tayari zimeshawekwa saini na Waziri anayehusika kwa ajili ya kuanza kutumika kwa mujibu wa Sheria.

Mhe.Mwenyekiti**,** kitendo cha Waziri kutunga Kanuni hizi na kuweka saini yake kwa ajili ya kuanza utekelezaji ni kutimiza matakwa ya Sheria ya Serikali za Mitaa, Namba 7 ya mwaka 2007 ambayo katika kifungu cha 94 kimemtaka waziri kutunga kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya Sheria hiyo. Niongeze kufahamisha kuwa uwezo wa kutunga sheria za nchi hii umepewa chombo maalumu ambacho ni Baraza la Wawakilishi kwa mujibu wa kifungu cha 88 cha Katiba ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, Baraza la Wawakilishi, kama ilivyo kwa mabunge mengine ya Jumuiya ya Madola, linakasimu madaraka yake kwa mawaziri na vyombo vyengine vya serikali kutunga Kanuni na Sheria ndogo ndogo kwa ajili ya kufafanuwa kwa undani zaidi utekelezaji wa Sheria husika. Kwa mnasaba huo Kanuni za Huduma za Serikali za Mitaa zimetungwa na waziri kwa nguvu aliyopewa na sheria ambayo imetungwa na Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo inachokifanya ni kutekeleza majukumu yake ya kuhakikisha kuwa uwezo aliokasimiwa waziri au chombo chengine wa kutunga Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo unatekelezwa ipasavyo bila ya kukiuka masharti ya Katiba, Sheria mama, Sheria nyengine na Kanuni nyenginezo.
Mhe. Mwenyekiti, Kanuni ya Huduma za Serikali za Mitaa ya mwaka 2017 imepitiwa na kuchambuliwa na Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo kwanza kwa kuipitia Sheria mama ya Serikali za Mitaa namna 7 ya mwaka 2014 ili kubaini masharti yaliyotowa mamlaka kwa waziri kutunga kanuni hizo kama yametimizwa kama inavyopasa (*delegated powers*). Kamati imejiridhisha

kuwa masharti ya kifungu cha 94 cha sheria hiyo yametimizwa na Mhe. Waziri anayehusika na ametekeleza wajibu wake kama ilivyoelekezwa na sheria. Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo inampongeza Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ kwa kutekeleza wajibu wake huo wa kisheria.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo baada ya kujiridhisha katika hatua hiyo imepita na kuchambua Kanuni za Huduma za Mamlaka ya Serikali za Mitaa za 2017 na kubaini mapungufu kadha katika kanuni hizo na ambayo tumeyaainisha kwa uwazi katika ripoti yetu iliyowasilishwa kwenu Waheshimiwa Wajumbe. Hivyo, napenda nichukuwe fursa hii nieleze japo kwa ufupi kama ifuatavyo:-

i. **Ushirikishwaji wa Wadau katika Utungaji wa Kanuni**

Mhe. Mwenyekiti, suala hili ni la jumla, kamati imebaini kuwa ushirikishwaji wa wadau mbali mbali kabla ya kutungwa kanuni hizi ulikuwepo lakini siyo wa kiwango cha kuridhisha. Kanuni hizi zinahusu uwekaji wa viwango vya ada, tozo na malipo mengine mbali mbali ya huduma zinatolewa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa ambazo hutoa huduma kama vile usafi, maegesho ya vyombo vya moto, usimamizi wa maeneo ya wafanyabiashara, wajasiriamali, wakulima, wavuvi, biashara ya usafirishaji abiria na mizigo kwa nchi kavu na baharini, mama na baba lishe, wasukuma marikwama, utalii na wafanyabiashara kwenye masoko na kadhalika.

Mhe. Mwenyekiti, kanuni hizi zinagusa sehemu kubwa sana ya maisha ya mwananchi mmoja mmoja popote pale alipo katika nchi yetu. Hivyo, ingetegemewa sana kuona kuwa wakati wa kutunga kanuni hizi kunakuwa na ushirikishwaji mpana sana wa wananchi ambao ndiyo walengwa watakaotozwa ada na tozo hizo.

Mhe. Mwenyekiti, kamati imebaini kuwa ushirikishwaji wao haukuwa wa kiwango cha kuridhisha na huenda utekelezaji wa kanuni hizo ukakumbwa na changamoto kadhaa. Hata hivyo, baada ya kukaa na waziri na watendaji wake tumejadiliana na kufahamishana na kutoa mapendekezo yetu, na wizara wamepokea mapendekezo hayo kwenda kuyafanyiakazi. Kwa niaba ya kamati napenda nichukuwe fursa hii kumshukuru sana na kumpongeza waziri anayohusika na wizara hii na watendaji wake kwa mashirikiano makubwa aliyotupatia. (*Makofi*)

ii. **Makosa ya Kiuandishi na Kiuchapaji**

Mhe. Mwenyekiti, katika ripoti yetu tumebainisha mapungufu kadhaa yaliyomo katika Kanuni za Huduma za Mamlaka za Serikali za Mitaa za mwaka 2017 ambayo ni makosa ya kiuandishi na kiuchapaji. Kamati tumeyabainisha mapungufu hayo kwa vile uandishi wa sheria au kanuni zenye makosa kama hayo kunaweza kuleta athari kubwa sana, kama vile kutofahamika maudhuwi ya sheria au kanuni kwenye kifungu husika, kuleta mchanganyiko wa maana kwa baadhi ya maeneo, maneno na sentensi (*ambiguity*) ambazo zinaweza zikapotosha maana halisi ya maneno iliyokusudiwa. Athari nyengine za makosa ya kiuchapaji na kiuandishi ni uwezekano wa kujitokeza mikinzano pindi yakitokea mabishano mahakamani ambako ndiko sheria zinakotafsiriwa.

Mhe. Mwenyekiti, tumebainisha makosa hayo katika ripoti yetu na wajumbe wanaweza kufanya rejea, lakini pia tulipata fursa ya kujadiliana na Mhe. Waziri na watendaji wake na kutoa mapendekezo yetu ambayo wizara wameyachukuwa na kwenda kuyafanyiakazi. *(Makofi)*

iii. **Ada na Tozo Zinazotumika katika Sheria na Kanuni za Zamani**

Mhe. Mwenyekiti, kamati imebaini kuna tozo na ada zilizowekwa katika Kanuni za Huduma za Mamlaka ya Serikali za Mitaa bado zinaendelea kutumika katika sheria nyengine; mfano wa ada hizo ni ada za leseni za madereva, matingo na vibali vya njia na ada za udhibiti wa mazao ya misitu na kadhalika.

Kamati imeona kuwa hatua hii inaweza kuleta usumbufu kwa wananchi wanaotozwa ada na tozo hizo ambao wanaweza kujikuta wanatozwa ada hizo na taasisi mbili tofauti ama viwango hivyo vya ada vikawa vikubwa kuliko walivyokuwa wakilipa hapo awali.

Mhe. Mwenyekiti, kamati ilipowaita na kujadiliana na wadau hasa wajasiriamali kama vile wafanyabiashara wa sokoni, mama na babalishe na wadau wa Sekta ya Usafirishaji wa Abiria na Mizigo (wenye daladala) walionesha kulalamikia utaratibu huo na kushauri kuwa serikali ifanye utarataibu wa kuweka pamoja ada hizi kwenye mamlaka moja, pamoja na kuweka unafuu wa tozo na ada ambazo kwao wanahisi ni kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, wadau hao waliomba kamati ifikishe kilio hiki kwa serikali, kwa kuitaka kufikiria kuwekwa unafuu wa viwango vya ada na tozo hizo ili wamudu kulipa bila matatizo yoyote, na lile lengo la serikali la kuwakwamua kiuchumi wananchi wake liweze kufikiwa.

C. KANUNI ZA MIRATHI YA KIISLAMU

Mhe. Mwenyekiti, kamati pia imepata nafasi ya kupitia na kuchambua Kanuni za Mirathi ya Kiislamu. Kanuni hizi zimetungwa na Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kutokana na uwezo aliopewa chini ya Kifungu cha 67 (1) cha Sheria Namba 2 ya mwaka 2007, Sheria ya Kamisheni ya Wakf na Mali ya Amana, Kanuni ambazo zimetangazwa katika Gazeti Rasmi kupitia Tangazo la Kisheria namba 55.

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kupitia na kuchambua kanuni hizi Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo imepitia Sheria Namba 2/2007, Sheria ya Kamisheni ya Wakf na Mali ya Amana na kujiridhisha kuwa kanuni hizo zimetungwa kutokana na masharti ya sheria hiyo. Aidha, samati imetazama uwezo aliopewa waziri wa kutunga kanuni mbali mbali katika sheria hiyo na kubaini yapo maeneo mengine ambayo waziri ametakiwa kuyatungia kanuni.

Mhe. Mwenyekiti, kamati imebaini mambo kadhaa wakati wa kupitia na kuchambua Kanuni za Mirathi ya Kiislamu, ambayo yameelezwa kwa uwazi katika ripoti waliyopewa wajumbe wa Baraza lako tukufu. Hata hivyo, naomba nichukuwe fursa hii kuelezea kwa ufupi.

i. Maeneo Yanayopaswa Kutungiwa Kanuni

Mhe. Mwenyekiti, kamati ilipopitia sheria namba 2/2007 ambayo ndiyo msingi wa Kanuni za Mirathi ya Kiislamu imebaini kuwa sheria hiyo imeainisha maeneo yanayohitaji kutungiwa kanuni, ili kuleta utekelezaji bora wa sheria hiyo. Mhe. Mwenyekiti, maeneo ambayo tumeyabaini ambayo yalipaswa kutungiwa kanuni, yametajwa katika kifungu cha 4 cha sheria hiyo kama yafuatavyo:-

a) Kusimamia Mali za Wakf, Mali za Amana na Mali za Maiti;
b) Kuratibu Shughuli za Hija zinazohusu Mahujaji kutoka Zanzibar na Kuratibu watu binafsi, taasisi au vikundi vinavyotoa huduma za kusafirisha mahujaji;
c) Kuratibu na kuweka utaratibu wa kikanuni kuhusu utoaji, ukusanyaji na ugawaji wa Zakka na Sadaka ambazo zinazotolewa kwa madhumuni ya kidini na misaada ya kheri; na
d) Kuratibu Sala na Mabaraza ya Iddi ya Kitaifa.

Mhe. Mwenyekiti, katika maeneo hayo tuliyoyabaini tumepata maelezo kutoka wizara kuwa yapo katika hatua mbali mbali ya kuandaliwa kanuni zake, kama tulivyobainisha kwa kirefu katika Ripoti ya Kamati ambayo wajumbe wanayo. Hata hivyo, kamati inapenda kuchukuwa fursa hii tena kuishukuru Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kuharakisha na kukamilisha hatua hizo za utungaji wa kanuni hizo, ili

utekelezaji wa Sheria Mama uwe bora zaidi, ili wananchi wetu wasipate usumbufu.

ii. Mgongano wa Baadhi ya Vifungu vya Kanuni na Sheria Nyengine

Mhe. Mwenyekiti, katika Kanuni ya 15 ya Mirathi ya Kiislamu imewekwa viwango vya adhabu na faini. Kamati imebainikia kuwa kanuni hiyo inagongana na kifungu cha 42 (e) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria yaani (*Interpretation Act*) Namba 7 ya mwaka 1984 ambacho kimeweka muongozo kuwa, adhabu ya namna hiyo isizidi faini ya Shilingi 7,000 au kifungo kisichozidi miaka miwili, au vyote viwili faini kama hiyo na kifungo kama hicho.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nirudie. Katika kifungu cha 15 cha Kanuni ya Mirathi ya Kiislamu, imewekwa viwango vya adhabu na faini. Kamati imebaini kuwa kanuni hiyo inagongana na kifungu cha 42(e) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria yaani (*Interpretation Act)* namba 7 ya mwaka 1984, ambacho kimeweka muongozo kuwa, adhabu ya namna hiyo isizidi faini ya shilingi 7,000 au kifungo kisichozidi miaka miwili, au vyote viwili yaani faini hiyo na kifungo kama hicho.

Mhe. Mwenyekiti, kamati imepata maelezo kuwa kanuni hiyo imefanya rejea ya Kifungu cha Sheria Mama ambacho kimeweka adhabu kama hiyo. Hata hivyo, Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo inashauri kuwa kanuni nyengine zitakazotungwa, zifanye mazingatio ya kutazama kigezo hicho na hilo liende sambamba na kufanywa marekebisho ya Sheria ya Tafsiri, ambayo baadhi ya masharti yake yameshapitwa na wakati ikiwemo kifungu hicho cha 42 (e).

iii. Makosa ya Kiuandishi, Kiuchapaji na Tafsiri ya Maneno

Mhe. Mwenyekiti, eneo jengine ambalo Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo imebaini ni mapungufu kadhaa kwenye uandishi, uchapaji na tafsiri ya maneno kama tulivyoainisha kwenye jadweli ya ripoti yetu. Tumejadiliana na wizara na kuyabainisha maeneo kadhaa yenye mapungu hayo kama yanavyonekana kwenye ripoti. Makosa hayo ya kiundishi, kiuchapaji na tafsiri sahihi ya meneno tumeshaeleza athari zake endapo kama yataendele kubakia kwenye kanuni. Kamati inasisitiza tu kufanyiwa marekebisho makosa hayo ili Kanuni zisomeke vizuri kwa watumiaji.

Mhe. Mwenyekiti, mbali na maeneo hayo, kamati imepitia Jadweli zilizoambatanishwa na kanuni hizo ambazo yapo maeneo kadhaa kama tulivyotaja kwenye ripoti ambayo yanahitaji kufanyiwa marekebisho. Mfano

wa maeneo hayo ni kuchanganya lugha ya Kingereza na Kiswahili kwenye baadhi ya maneno kunaweza kuleta matatizo ya uwelewa na tafsiri sahihi. Tunashukuru na tuipongeze sana wizara kwa kupitia Mhe. Waziri, kwa kuweza kuyapokea mapendekezo yetu kwa ajili ya kwenda kuyafanyiakazi.

D. KANUNI ZA MAKAMPUNI ZA MWAKA 2017

Mhe. Mwenyekiti, wakati tunaelekea katika maandalizi ya ripoti hii, kamati yangu imepata kupitia Kanuni za Makampuni za mwaka 2017 ambazo zimetungwa na Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko kutokana na uwezo aliopewa chini ya Kifungu cha 277 (3) cha Sheria ya Makampuni, Sheria namba 15 ya mwaka 2013. Kanuni hii imeletwa katika kamati yetu katika muda ambao ripoti ya uchambuzi juu ya kanuni hizi ipo katika hatua za uchapaji. Kwa hivyo, tumeitaja tu ndani ya muhutasari wa ripoti yetu na maelezo ya nini kamati imebaini katika kanuni hizi, tutayaeleza kwa ufupi tu katika hotuba hii.

Mhe. Mwenyekiti, tunawaomba sana radhi Waheshimiwa Wajumbe, kutokana na kutokuwepo kwa uchambuzi wa yale tuliyoyabaini katika kanuni hizi za makampuni, kwa sababu kanuni hii imekuja katika kipindi hiki ambacho Baraza linaendelea.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kamati kukaa na uongozi na watendaji wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kujadili Kanuni za Makampuni za mwaka 2017, mbali ya mambo mengine, kamati imebaini kuwa ushuru wa stempu yaani *stamp duty* wa asilimia 0.5 ya mtaji wa kampuni unaotozwa na Bodi ya Mapato Zanzibar (*ZRB*) wakati wa usajili wa makampuni hauna kikomo hivyo hupelekea watu wengi wanaotaka kusajili kampuni zao hususani wageni kushindwa kusajili kampuni zao au kufanya udanganyifu kwa kuweka kiwago cha chini cha mtaji wa kampuni zao ili kuepuka kiwango kikubwa cha kodi hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuliangalia vizuri suala hili ili nchi yetu iendelee na iweze kuwashajihisha wawekezaji kuja kuwekeza nchini na si kuweka vikwazo vinavyorudisha nyuma maendeleo yetu kwani uzoefu wa nchi nyengine ikiwemo nchi ya Rwanda unaonesha kodi ya aina hiyo imeondolewa na hatimae wawekezaji wengi wamevutiwa kuwekeza nchini humo. Hali hiyo hupelekea Serikali kupata mapato mengi baada ya kampuni hizo kuanza kufanya kazi. Hivyo, Kamati inashauri Serikali kuondoshwa kwa kodi hiyo ya 0.5% inayotozwa wakati wa usajili wa kampuni hapo itakapo jadiliwa na kukubalika.

Mhe. Mwenyekiti, Aidha, Kamati imefurahishwa sana na majadiliano na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa ufafanuzi wao juu ya hoja zilizotolewa pamoja na kukubaliana na mapendekezo yaliyowasilishwa na Kamati likiwemo lile la kuzitafsiri Kanuni hizo katika lugha ya Kiswahili jambo ambalo litarahisisha kufahamika kwa Kanuni hizo. Hivyo, Kamati inaiomba Serikali kuipatia fedha za kutosha Wizara husika hiyo ili iweze kufanikisha azma yake hiyo itakayoleta manufaa kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti**,** Hata hivyo, nichukuwe fursa hii kumshukuru Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko na watendaji wake kwa mashirikiano waliyotupa katika kikao cha kujadili uchambuzi wa Kanuni yao ya Makampuni na kwa uungwana wao wa kukubali kuyapokea mapendekezo ya Kamati kwa lengo la kuyafanyiakazi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nikiri kuwa Kanuni za Makampuni zimetengenezwa vizuri na Kamati haijabaini mapungufu yoyote yanayokinzana na Katiba, Sheria mama na Sheria nyengine za nchi. Kwa ujumla kamati imebaini tu baadhi ya maeneo kadhaa yenye mapungufu ya kiuandishi, kiuchapaji na mlingano *consistence* wa maneno kwenye vifungu vya Kanuni na Majadweli hayo ambayo Wizara itayafanyia kazi.

MAONI NA USHAURI WA KAMATI KUHUSU KANUNI TILIZOCHAMBULIWA

Mhe. Mwenyekiti, kwa ujumla baada ya mapitio ya Kanuni zote hizo (3) Kamati yangu inaomba kuwasilisha maoni na ushauri ufuatao kwa taasisi zote za Serikali zinazohusika na Utungaji wa Kanuni:-

Mhe. Mwenyekiti kwanza:

a. Kamati inashauri kutoa ushirikishwaji mpana kwa wananchi katika hatua za awali za utungaji wa Kanuni;

b. Lakini vile vile kuwashirikisha Wanasheria wa ndani wa Taasisi hizo katika hatua zote za utungaji wa Kanuni hizo; na hata Kama Taasisi italazimu kutafuta Mtaalamu kutoka nje basi ni muhimu Mwanasheria wa ndani akaambatanishwa na mtaalamu huyo/wataalamu hao kutoka ili kupata uzoefu na kuweza kujifunza masuala mazima ya kuweza ya kutunga kanuni.

c. Lakini ushauri mwengine Mhe. Mwenyekiti, kamati inashauri kanuni zitungwe kwa lugha ya Kiswahili na kutafsiriwa kwa lugha ya kiingereza, aidha matumizi ya lugha fasaha na sahihi yazingatiwe kwa umakini mkubwa ili kuepusha mapungufu ya Kiuandishi, Kiuchapaji na kimantiki. Kwa mfano; Kanuni ya Makampuni ya mwaka 2017 kanuni hii Mhe. Mwenyekiti

imetungwa kwa lugha ya Kiingereza, hivyo tunashauri kanuni hiyo itafsiriwe kwa lugha ya Kiswahili ambayo ndiyo lugha inayoeleweka na watumiaji wengi wa Kanuni hizo.

d. Mhe. Mwenyekiti, Ushuri mwengine ambao Kamati inatoa yawepo mashirikiano makubwa na ya karibu baina ya Taasisi zinazohusika na utengenezaji Sheria kama vile Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, Tume ya Kurekebisha Sheria, Wakala wa Serikali wa Uchapaji na Taasisi na nyengine za Idara za Serikali, Mashirika, Mamlaka ya Serikali za Mitaa n.k Kamati tumebaini kuwa wakati mwengine Kanuni zinachelewa kutungwa kutokana uwepo wa mashirikiano hafifu yaliyopo na Taasisi mbali mbali.

MAPENDEKEZO YA JUMLA YANAYOHUSU UTENDAJI KAMILI WA KAMATI

Mhe. Mwenyekiti, Sasa niruhusu nitowe mapendekezo ya jumla yanayohusu utendaji kamili wa Kamati yangu ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo.

Mhe. Mwenyekiti sasa naomba nitoe ya Kamati katika maeneo mbali mbali tuliyoainisha katika ripoti yetu kwa utaratibu ufuatao:-

a. KUIJENGEA UWEZO KAMATI

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo inapendekeza ijengewe uwezo wa Kutekeleza majukumu yake kwa kupatiwa ziara za mafunzo katika mabunge mengine mfano; Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kujifunza kwa vitendo namna ya kufanya mapitio na uchambuzi wa Kanuni kwa kina zaidi na ufanisi. Sambamba na hilo, tunapendekeza kujengewa uwezo wa kipekee Sekretarieti ya Kamati hii ambayo ndiyo yenye kazi kubwa ya kufanya maandalizi ya kupitia na kuchambuwa sheria mama, katiba, sheria nyenginezo na kanuni zake, kabla ya kuwasilisha kwa Kamati. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, tunaomba sana Ofisi ya Baraza la Wawakilishi kufanya kwa makusudi ya kuiwezesha Sekretarieti hii kuipatia fursa ya kupata mafunzo zaidi ya kuijengea uwezo ili iweze kuisaidia Kamati kwa weledi zaidi. Kwa hatua ya sasa tunaishukuru Sekretarieti yetu kwa mashirikiano na wajumbe wote na Kamati wameweza kutekeleza majukumu yao kama ilivyotakiwa. *(Makofi)*

b. UFANISI KATIKA UTENDAJI KAZI WA KAMATI

Mhe. Mwenyekiti, katika kuongeza ufanisi wa utendaji kazi Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo; Kamati yetu inapendekeza Baraza la Wawakilishi

kuweza kufanya marekebisho ya Kanuni ya 33(4) ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, toleo la 2016 ambayo inaleta kikwazo kwa Kamati katika kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mhe. Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika Kamati hii inailazimika kuweza kuzipitia Kanuni na sheria ndogo ndogo ndani ya kipindi cha miezi mitatu tangu kuchapishwa kwenye Gazeti Rasmi la Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, Kanuni hiyo kama itabakia ilivyo huenda kanuni ya Kamati na Sheria Ndogo Ndogo ikajikuta haifanyi kazi yoyote kwa vile inawezekana wakati Kamati inapanga kazi za kupitia Kanuni na Sheria ndogo ndogo ikawa ishapitiwa na muda wa miezi mitatu tokea kuchapishwa kwake. Lakini zaidi.*(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Kanuni hii inainyima fursa Kamati kupitia Kanuni na Sheria ndogo ndogo za nyuma ambazo pengine zimetungwa bila kuzingatia masharti ya Sheria mama, Katiba na Sheria nyengine. Aidha wakati mwengine zikawa utekelezaji wake unalalamikiwa na Wananchi wetu.

d. UTUNGAJI WA KANUNI NA SHERIA NDOGO NDOGO KWA WIZARA NA TAASISI ZAKE

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu inachukuwa nafasi hii kuzijulisha Wizara, Idara na Taasisi zote za Serikali kutambuwa kuwa Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo ipo na inafanyakazi zake za kupitia na kuchambua Kanuni na Sheria ndogo ndogo. Hivyo basi, Taasisi zote hizo zihakikishe kuwa mara tu baada ya kutunga Kanuni kuweza kuwekwa saini na Waziri husika na kutangazwa katika Gazeti Rasmi la Serikali, zinawasilishwa Kanuni mbele ya Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo kwa ajili kupitiwa kwa mujibu wa Kanuni.

Mhe. Mwenyekiti, tunapendekeza pia katika ripoti yetu Kamati za Kisekta za Baraza la Wawakilishi zinapokuwa katika Kazi zao za kawaida za kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara zao basi, kuzitambuwa Sheria zinazosimamiwa na Wizara hizo na kuhakikisha kuwa Kanuni za sheria hizo zinatungwa ndani ya mwaka wa fedha. Sambamba na hilo, Wizara zote zihakikishe mara tu sheria inapopitishwa na Baraza basi Kanuni zake zitungwe ndani ya mwaka wa fedha unaohusika.

HITIMISHO

Mhe. Mwenyekiti, napenda nimalizie kwa kubainisha kuwa katika mapitio ya Kanuni zote hizo tulizozitaja hatujakuta jambo lolote kubwa kinyume na katiba, sheria mama au sheria nyengine ambazo lingepelekea Kamati yangu

itowe au ipendekeze azimio maalumu ndani ya Baraza hili la kubatilisha Kanuni hizo. Kwahiyo tuzipongeze Wizara zote ambazo zimeleta kanuni kwetu. Mapungufu tuliyoyaona ambayo tumeyaeleza hapo awali zaidi tumekaa na Wizara zote zinazohusika na kutoa mapendekezo yetu ya namna bora ya kuyashughulikia kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Baraza zinazohusika.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ujumla Kamati yetu imefanyakazi zake zote hizo ikiwa ni sehemu ya kazi za kawaida pamoja na mafunzo ya kujiongezea uwezo. Tumefanyakazi kwa mashirikiano makubwa na Ofisi ya Baraza la Wawakilishi ambayo imeratibu mafunzo ya awali na kuijengea uwezo Kamati yetu. Tunamshukuru sana Katibu wa Baraza na Watendaji wake Wakuu wa Idara na Divisheni kwa mashirikiano waliyotupa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mara nyengine vile vile nichukuwe fursa hii niwashukuru Mawaziri na watendaji wote wa Wizara ambazo Kanuni zao zimepitiwa na kamati yangu kama nilivyotangulia na kuzitaja kwenye utangulizi wa hotuba hii. Kwa dhati kabisa wametupa mashirikiano makubwa na tumejadiliana vizuri na kwa hakika tumejifunza mambo mengi kutoka kwao na imani ya kamati yangu kwamba mashirikiano hayo yataendelea. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, napenda vile vile nichukue tena fursa hii ya kuwashukuru Wajumbe kamati yangu na Makatibu wangu wa Kamati kwa mashirikiano makubwa ambayo wameipatia kamati hii hadi kuweza kukamilisha na kuweza kuwasilisha kwa ripoti hii.*(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa nikushukuru wewe kwa kuwa karibu na kamati zako za Baraza ikiwemo Kamati yetu, kwa miongozo na ushauri wa Mhe. Spika unaotufanya tutekeleze majukumu yetu kwa ufanisi zaidi. Aidha, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuwasilisha muhtasari huu mbele ya Baraza lako Tukufu.

Kwa ujumla nawashukuru wajumbe wote wa Baraza kwa kunisikiliza. Na kwa niaba ya Kamati yangu nawaomba Wajumbe watushauri, na ikiwezekana waweze kutuelekeze kwa vile kamati hii ripoti yetu hii ni ya kwanza kabisa kuwasilishwa katika Baraza letu tukufu. *(Makofi)*

Nawashuku sana wajumbe wote na NAOMBA KUTOA HOJA. Ahsanteni sana. *(Makofi)*
Mhe. Mwenyekiti, baada ya uwasilishwaji wa ripoti hii ya Kamati yangu ya Kanuni sasa naomba uniruhusu namie nichangie machache ili kuweza kuunganisha na ile michango ya waheshimiwa wajumbe watakayoitoa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nije katika fanisi katika utendaji kazi wa kamati.

Mhe. Mwenyekiti, katika ripoti yanagu nilizunguzia juu ya kanuni ya 33(4).

Mhe. Mwenyekiti, kanuni hii kwa kweli ni kiwazo kwa kamati, lakini pia kwa wajumbe wale ambao wataka walete mapendekezo ya marekebisho ya kanuni barazani kwa mujibu wa kanuni ndani ya kipindi cha miezi 3, kamati tokea kuchapishwa na kutiwa sanini kwa kanuni ndio kipindi ambacho kamati hutakiwa kuweza kufanyakazi zake.

Mhe. Mwenyekiti, kipindi hichi ni kipindi kifupi sana lakini vile vile kama tulivyotangulia kusema kama inakuwa ni kikwazo kuweza kuzichambua kanuni za nyuma ambazo pengine wakati mwengine zinalalamikiwa na wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, ndani ya kipindi hichi ambacho ambacho tulichambua kanuni za makampuni.

Mhe. Mwenyekiti, kanuni za makampuni zimekuja mwezi uliopita, sasa kutokana na kikwazo kwa kanuni ya 33(4) tulilazimika kamati iweze kukaa na kuweza kuifanyia kazi kanuni hii. Kwa hiyo ilitupa ugumu sana huku tufanye kazi za baraza na huku tuweze kukaa na wahusika katika kuichambua na baadae kuitolea maoni kanuni hii, na ndio maana katika ripoti ambayo tumewasilishia wajumbe, hamna yale mapendekezo juu ya mapungufu juu ya kanuni hii ya makapuni.

Mhe. Mwenyeti, sasa naomba baraza liweze kufahamu ugumu na kikwazo cha kanuni hii kanuni hii kama itarekebishwa inaweza ikaipa uhuru kamati kuweza kufanyakazi kwa utulivu na uweledi mkubwa lakini vile vile ikaweza kupata fursa ya kuweza kupitia hata zile kanuni za zamani ambazo pengine zinaletwa kikwazo kwa walengwa.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo nije kwenye suala zima la sheria za tafsiri.

Mhe. Mwenyekiti, Sheria ya Tafsiri ya Sheria (*interpretation act.* No. 7 ya mwaka 1984) ukweli sheria hii Mhe. Mwenyekiti ni ya muda mrefu, sheria hii ishapitwa na wakati inahitaji marekebisho ya vifungu mbali mbali, athari na vikwazo katika sheria na kanuni zinakuwa zinajitokeza sana kutokana na kutofanyiwa marekebisho ya sheria hii kama nilivyotaja katika hotuba yangu kwa mfano kile kifungu cha 42(e). Sasa niombe sana serikali na nimuombe sana Mhe. Mwanasheria Mkuu ambae niliwahi kuzungumza nae juu ya kadhia ya kupitiwa muda na sheria hii ya tafsiri.*(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie michango yangu juu ya suala zima la kuchelewa kwa utungaji wa kanuni.

Mhe. Mwenyekiti, lengo la kanuni ni kuweza kusimamia utekelezaji wa bora wa sheria sasa pale ambapo kanuni hizi zinachelewa kwa kweli tutakuwa tunawakwaza wananchi wetu kwa sababu sheria ambazo zinatungwa maana yake sheria hizi lazima ziwe na nyezo nyengine ambazo ndio kanuni na baada ya kanuni ndio ambayo unaweza ukatoa miongozi mbali mbali. Kwa hiyo kuchelewa kutungwa kwa kanuni za sheria mbali mbali tunazipitisha hii itakuwa ni kikwazo.

Kwa hiyo kwa niaba ya kamati yangu niiombe sana serikali na hususan wale mawaziri na vyombo vyengine ambavyo vinakasimiwa madaraka haya kutunga, basi kuweza kuharakisha pale ambapo sheria zinatungwa basi na wao wasichukuwe muda waweze kuzitungia kanuni ili kuwa na utekelezaji bora kabisa kwa sheria ambazo tunatunga lakini vile vile kuwaondolea usumbufu wananchi wetu na sheria hizi ziweze kutekelezeka vizuri, katika sualala zima lile lile la madhumuni makubwa sana ya utawala bora wa sheria.

Mhe. Mwenyekiti, nishukuru sana kwa kuniruhusu na mimi kuchangia na nichukue fursa hii niwashukuru na niwapongeze sana wajumbe na niwaombe sana na jua kwamba ripoti hii inahusiana sana na mambo ya kanuni na sheria na wakati mwengine yana ugumu wake, lakini niwaombe sana ndugu wajumbe waichangie hotuba hii vizuri kwa maslahi ya taifa letu.

Ahsanteni sana kwa kunisikiliza.*(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe.Rashid Makame Shamsi, Mwenyekiti wa Kamati ya Kanuni na Sheria ndogo ndogo kwa ripoti yako.Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa na imeungwa mkono, majadiliano yanaendelea, kabla sijamwita mchangiaji wetu wa mwanzo naomba tutambue ugeni ulioingia hivi punde.

Wageni hao ni wa Mhe. Rashid Ali Juma Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo. Wageni hawa wanatoka *World Kick Boxing Network*, jumla yao ni wanne nao ni:-

1.	Mr. Stephano Cabrera	Rais wa Dunia wa Michezo ya Kick boxing
2.	Mr. Othman Igin	Bingwa wa dunia Kick Boxing
3.	Mr. Emanuel Mlundwa	Mkurugenzi wa *PST* ambae pia Mwakilishi wa *World Kick Boxing Network* kanda ya Afrika

4. Ndg. Ashraf Suleiman Bingwa wa *World Kick Boxing Tanzania (Makofi)*

Karibuni sana. Waheshimiwa tunaendelea sasa naomba nimwite mchangiaji wetu wa mwanzo Mhe. Suleiman Sarahan Said, atafuatiwa na Mhe. Ali Salum Haji na Mhe. Ame ajiandae.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti na mimi kunipatia fursa hii ya kuchangia machache katika ripoti ya Kamati ya kudumu ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza niipongeze sana kamati pamoja na Mwenyekiti katika kutuwasilishia ripoti hii, lakini pia kitabu chake alichokiandika kwa ufundi mkubwa na ustadi nimpongeze sana, kwa sababu hiki kitabu ni cha sheria zaidi kuliko mazungumzo zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niende kwanza katika ukurasa wa nne ambapo kuna jambo hapa nimeliona katika kifungu cha tatu uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa katika mkutano wa saba wa Baraza la Wawakilishi, kuna Kanuni zinazozungumzia mamlaka ya Serikali za Mitaa na kuna Kanuni za mirathi ya Kiislamu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naanza na hapa kwenye mirathi. Kwa kweli shughuli zote za mirathi na mambo mengine katika Kanuni na Sheria za Kiislamu zimemalizika sana, mambo mengi pale Uislamu umemaliza na wanaweza wakafanyia mambo yao sana. Lakini mimi nilipofurahi kuja kuziangalia hizi Kanuni kwa upande wa serikali nimefurahia sana.

Mhe. Mwenyekiti, familia zetu karibu asilimia sabini zinakuwa na matatizo ya mirathi ama watu hawarithi kabisa, ama inakuwa ukidai urithi wako inakuwa ni mashaka makubwa kweli kweli. Mimi nimefurahi sana kuona kwamba kutakuwa na Kanuni ambazo zitasaidia kusukuma hali hii ya mirathi. Sisi unatukuta muda wote mtu anafanya mambo yake lakini tumesahau kile kile kitabu chetu cha Quran kilichosema na pamoja katika hadithi za Mtume (SAW) kwamba mtu akifa arithiwe, lakini sisi haturithi. Kwa hivyo tukiangalia hapa mimi nafurahi hizi Kanuni zikitungwa, napenda kwamba zinasaidia kusukuma watu katika kuweka haki zao za msingi. Kwa hivyo hii nilikuwa naitilia maanani kwamba nafurahi kuona serikali kwa sababu ina miongozo zaidi pamoja na kwamba kuna Sheria za Kiislamu lakini pia kukawa na *force* kidogo ya watu kuwekwa katika haki zao. Ningependa sana hili suala lilivyo kwa sababu upande wa mirathi una matatizo sana, mtu akidai haki zake mashaka na haki yake inapotea na wengine wanakula haki ambazo si zao. Kwa hivyo hili litasukuma kuweka mirathi sawa katika mambo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika ukurasa wa nane, kuna viwango vya adhabu kwa makosa mbali mbali. Hapa nimeona nilisema kwamba vipunguzwe na hasa ukizingatia watumiaji, wahusika wengi wa Kanuni hizi ni maskini, mfano wajarisiamali wadogo, mama na baba lishe, watembeza bidhaa, wavuvi na kadhalika.

Mhe. Mwenyekiti, hapa kama ilivyosema kamati ni kweli, sheria nyingi tunazitunga kwa mdomo tu lakini bila kuangalia hali halisi ya maisha ya mtu, lakini pia nyengine tunazifanya kama ni adhabu ya kumkomoa mtu ambazo hazitizami hali halisi ya masuala husika ambayo nini tunachokifanya, tunakomoana kupita kiasi kwa sababu sheria zenyewe anazitoa mtu bila kutizamwa na jamii au kufatiliwa. Lakini pia kutokana na kitabu hiki kilivyoandikwa ni kwamba hizi sheria zinatungwa lakini hazishirikishi wale watumiaji wa sheria zile ambao ndio walengwa au makundi fulani ambayo ndio yatahusika wakalitizama lile jambo kwa kina wakaliona lina umuhimu wake, lina sifa za kufanya kile kitu badala yake wanatunga sheria lakini zinakuwa ni kikwazo kikubwa sana kwa watu kuzitekeleza zile sheria. Huwezi ukamwambia mtu kwamba kitu kidogo kakosea ukamwambia utalipa laki moja papo kwa papo au uende jela pahali fulani, vitu vingingine vinakuwa *too much* vinakwaza sana, utakuta hata sheria za sasa hivi tulizonazo lakini wale watumiaji sheria pia hawafahamishwi.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi unaweza kwenda kwenye barabara maeneo ya *parking* ukapaki sivyo, akaja mtuchuma akakufungia, akishakufungia anaondoka anakimbia hasa anakwambia anamtia adabu. Sasa wewe umekwenda kumtia adabu mtu pale au unasimamia sheria, hawajui zile sheria, yeye kakufungia ni lazima ujue kitu kimoja, ufunguaji wake unamfahamisha anaupata wapi, wewe ndio utakayemfungulia, anakwenda kulipa, anakwenda kufanya nini umfahamishe.Yeye anaondoka anakimbia halafu hujui ufanye nini, sasa kama anakutia adabu kama lile jambo la kwake siyo la kisheria. Kwa hivyo mimi nafurahi sana sheria ndogo ndogo zikitungwa lakini pia na wale wahusika basi wafanyiwe marekebisho ya kuwa wanashirikishwa kupewa elimu au wanashirikishwa katika kutunga na kujua thamani yake.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye ukurasa wa kumi kuna baadhi ya kasoro zilizogundulika kama ifuatavyo, utaratibu uliotumika kwa kutunga kanuni hizi. Kuna sehemu inaitwa kifungu cha (a)

"Ushirikishaji wahusika wadau wakiwemo wananchi watarajiwa kwa kiasi kikubwa kutumia Kanuni hizo ulokuwapo ila kwa kiwango kikubwa, hivyo kamati imeishauri wizara kama nyengine itakapokuwa inatayarisha Kanuni na

kitu chochote ambacho kinaihusu jamii ni vyema ikaishirikisha jamii husika ili iwe rahisi katika utekelezaji wake"

Hii ndio niliyokuwa naizungumzia sana Mhe. Mwenyekiti. Sisi hizi Kanuni ndogo ndogo zinatungwa kwa kurahisisha au kwa kuweka vitu sawa katika jamii, na ikiwezekana kama mtu kakosea basi adhabu yake nayo iweze kutekelezeka isiwe kama kikwazo. Sasa mimi naipongeza sana katika kifungu hiki, katika sheria hii ni kwamba ni jambo la msingi sana katika maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, chengine nikija kwenye ukurasa wa kumi na moja kuna makosa ya kiuandishi na makosa ya kiuchapaji, hapa tunatakiwa tuwe makini sana. Sheria inapoandikwa kwanza tujue yule unaemtungia nani, unaandika sheria ndogo tu ya kufanya kitu katika sehemu unamuandikia Kiingereza, mtumiaji anatumia Kiswahili, yeye hajui atachambua vipi, masuala yake atayajua vipi, wewe unampeleka karatasi ya Kiingereza. Hapa lazima tutizame na tuwe wazalendo katika nchi yetu, siyo kwamba kuandika Kiingereza ndio kujua kusoma lakini ni kumfahamisha yule mtu. Kwa hivyo ningeomba maandishi ambayo yanakwenda kwa jamii basi yazungumze lugha ambayo wanaiofahamu kama ni Kiswahili kwa kwetu, lakini pia uchapaji ningeomba kabla ya kitabu na vitu vyengine kutoka basi kipitiwe ili kiweze kutoka bila kuwa na makosa ya kiuandishi ambayo haya ni makosa ya kisheria. Baadae inaleta kama mgongano fulani ambapo mpaka kiwe kimetoka au kimefanya vipi ndio mambo haya yanakuja kubadilika.

Mhe. Mwenyekiti, lugha ni haya maneno aliyosema pia ina sifa yake, lugha sasa hivi ya Kiswahili imekuwa pana sana, tunatumia maneno ambayo naweza kusema ukilijua usilijue lakini ndio litaingizwa katika mabano. Kwa hivyo ningeomba sana lugha fasaha ikaweza kutumika katika sheria zetu hizi ili isiwe kikwazo au isiwe jambo ambalo kwa mtu mwengine linaweza likamkwaza. Kwa hivyo ningeomba sana mambo haya ambayo wameyaona kamati, basi nayo ni kutiliwa maanani baina ya kiuandishi, kiuchapaji na pia katika maeneo ya lugha mambo haya nayo yakaweza kuwekwa sawa ili ushirikishaji na wahusika wenyewe wakaweza kuangalia.

Mhe. Mwenyekiti, tuna sheria nyingi hapa ambazo zinakuwa na mashaka mamoja katika mambo ya Dini na mambo ya sheria ndogo ndogo. Nimeona sana huku katika jaduweli hili na hii nimeipenda kitu kimoja Mhe. Mwenyekiti, sisi kama serikali tunatakiwa wananchi wote tuwafahamishe kitu gani ambacho kinatakiwa, tuwafahamishe jambo gani tunapolianzisha. Leo unawachia watu uhuru wote wanaokwenda Makka, kila mtu unampa ruhusa anayekwenda Makka afungue ofisi yake apeleke watu Makka. Matokeo yake hakuna mtu anayekwenda Makka, pesa zao zinaliwa, kila mtu anafanya analotaka, wengine hawafiki. Huu utaratibu tumeuanzisha sisi kama serikali, lakini tumetoa vibali,

tumetoa ruhusa sivyo, watu wamekuwa kila mmoja anapeleka tu. Kwa hivyo ningeomba hii nimeiona sana hapa Mhe. Mwenyekiti hii kamati hapa imepitia pazuri.

Mhe. Mwenyekiti, chengine ndio hii tuloizungumzia kusimamia mali za wakfu, mali za amana na mali za maiti. Hhiki kitengo chote kwenye Uislamu kimemaliza kila kitu. Narudia kusema tena lazima serikali nayo itie mkono wake wa kujenga Kanuni ndogo ndogo, ili kwa yule mtu ambaye haki yake haipati aweze kuipata, kwa sababu sijui niseme wenzetu kama Mashekhe wengine au kitu gani, wanajua kwamba mtu akifa warithi uwagawie mali zao, yeye ukienda kudai tu unaambiwa wewe ulikuwa unamuombea baba yako afe, au ulikuwa kitu gani, maana yake anakuzungusha tena. Sasa naomba hizi sheria zikikamata ukasema kwamba mtu akifa tu mali zake ziletwe zigaiwe, basi sheria zitasaidia kuwapa watu haki zao kabisa kabisa kuna utaratibu mwingi ambao mambo na hii ya Hijja kama alivyosema Mwenyekiti hapa, mpaka sasa hivi hakujatungwa sheria hazijatayarishwa za Hijja. Makosa yapo ya Hijja nimeyasikia kwenye mitandao kipindi kilichopita, watu wanatukanana utanilipa pesa zangu sijui utafanya kitu gani. Kwa hivyo serikali ichukue jukumu la Hijja kwamba kampuni gani ambazo zina uhakika wa kuwapeleka watu Hijja, siyo kila mmoja afungue ya kwake.

Mhe. Mwenyekiti, nyingine ni ukusanyaji wa zaka na sadaka. Hapa nimeambiwa imeshakamilika hii sera lakini bado utakuta malalamiko hayo hayo tunayozungumza kwamba sadaka na zaka zikija kwetu katika mambo mengi zinafikia mikononi mwa wajanja, hazifiki kunakohusika. Mhe. Mwenyekiti, zikitungwa hizi Kanuni na mambo yatakavyokuwa basi kila mmoja atapata haki yake katika masula ya utandawazi.

Mhe. Mwenyekiti, kuna suala la upande wa watoto au mimi sikuona hata upande wa watoto kama wamegusiagusia katika sheria ndogo ndogo. Mhe. Mwenyekiti, watoto wanasheria nyingi za kuwalinda pamoja na wazazi, lakini humu katika sheria ndogo ndogo zinakwazana kwazana baina ya sheria za serikali, sheria za Dini, basi na sheria ndogo ndogo hapa zingepitia katika mikono hii ya watoto angalau watoto nao wakaweza kuwa wana sheria ndogo ndogo za wazazi kuwabana au mtoto yule atawekwa katika mazingira gani.

Sasa sikuiona hapa katika maelezo hayo lakini tuna matatizo sana, kwa sababu hivi vitu vya jamii, ndio vilivyotungiwa hizi Kanuni ndogo ndogo, ni matatizo makubwa kwa watoto katika familia zetu. Mhe. Mwenyekiti, niliwahi kuuliza suala moja hapa nikauliza kuna sheria ya mtoto akifika miaka saba anapewa wazazi wake, wakasema aah! hakuna sheria hiyo wala kitu gani. Lakini sasa baba anataka mtoto, mama anataka motto, mwenye mtoto nani, na wote wawili wamezaa. Sasa hapa pakitungwa visheria vikaweza kubanabana tunampa

maisha yule mtoto badala ya kumkandamiza kwa wazazi wawili, serikali inaweza ikamuokoa yule mtoto kutokana na sheria ndogo ndogo. Sheria zetu zinakuwa za kuvutana, zikivutana mtoto tunamuathiri sana katika maisha yake. Mhe. Mwenyekiti, na hilo nilikuwa nataka niliseme kabisa tuangalie ushirikishaji.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, ninakuja kwenye ukurasa wa nane. Kuna suala la makosa ambayo kiwango, hizi sheria hakuna kosa lililokuwa halifanani na kosa mwenzake au hakuna kosa ambalo linakuwaje. Makosa mengine kama yakiwa kwenye Mahakama, pengine katika ratiba yake anaandikwa utalipa elfu kumi, isizidi elfu thelathini. Makosa yanayokuja haya kwenye Serikali za Mitaa, hawa watu wetu wa Manispaa, wale hawana msalie mtume, wale wakishapewa rungu, sheria zao wanazitunga wenyewe, wakafanya wanavyotaka wenyewe. Nashukuru tu siku hizi kidogo angalau kuna wanasheria wanasaidia nguvu kidogo haitumiki sana, lakini bado nasema tena bado kwenye Serikali za Mitaa bado kuna watu elimu yao ndogo, wanatumia vifua zaidi kuliko busara, anakufanyia mtu kama wewe siyo nchi yako, anakuharibia kitu anasema nenda unakotaka kwa sababu kuna sheria inayomlinda.

Mhe. Mwenyekiti, ningeshauri sana hizi sheria zikitungwa nazitungwe haraka iwezekanavyo ziwekwe vizuri na zipitiwe zilizopo ili kuonekana kwamba wakati, mimi nina uhakika kwamba kuna sheria bado zinaitia hasara. Maana kuna sheria nyingine sijui za kilimo huko utakuta mpaka leo mnazi ukiukata unalipa shilingi moja, pesa mbili, pesa nane. Ninajua sheria zipo huko ukitizama hata hazilingani tena. Lakini thamani ya mti haujulikani, unakwenda kuukata mti umeshatengenezwa mpaka kufika pale umeshagharimu pesa nyingi, watu wameutilia maji, faida yake kubwa, unaukata unaambiwa lipa shilingi ishirini au shilingi kumi. Kwa hivyo naomba kuna sheria nyingi ndogo ndogo katika wizara nyingi, bado zinahitaji zifanyiwe marekebisho kwa sababu ya wakati. Ningeomba sana suala hili na mimi naliunga mkono katika masuala ya kupitiwa kwa hizi sheria kila sehemu ambazo tunazo sheria ndogo ndogo tukazipitia kutizama na thamani.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, na hizi adhabu zilizowekwa, adhabu zaidi zinawekwa pale mahala ambapo pana mambo mengi. Kwa utaratibu huu tunaouweka wa sheria ndogo ndogo nashauri sana faini iwe bora zaidi kuliko kifungo. Maana yake tukisema tunampiga mtu na kifungo bila faini kwa sababu na serikali inataka mapato na wewe unahitajika kesho unataka ufanye tena kazi. Kwa hivyo naomba sana sheria zetu zika-*base* sana kwenye faini kuliko kifungo, kifungo kinakuwa tena ni hatua ya mwisho pindipo itakapokuwa hakuna uwezekano tena. Ningeomba hivyo na hizo faini zenyewe tuangalie maisha ya wananchi wetu, faini ile anaweza akaifanya hata mtu aliyekuwa maisha yake ya chini,

lakini inakuwa kuanzia siku ile akipigwa faini mwezi mzima hajaunga kafilisika tu yuko taabani.

Kwa hivyo ningeomba isitizame upande mmoja hizi sheria kwa elfu kumi nini, elfu ishirini nini, kwa watu wengine kubwa na pale hatuchagui mkubwa wala mdogo anayetaka kufanya. Kama itatungwa sheria basi ziweze kuwa *interval* ya kitu kama ni elfu isizidi elfu thelathini kutokana na hali itakayoonekana inafaa au mtu anajirudia rudia kwenye makosa inaonekana nini cha kufanya. Mhe. Mwenyekiti na mimi nilikuwa nachangia sana kuangalia hali za faini zisikwaze, ziweze kutekelezeka. Masuala ambayo tunakwenda kwenye jamii.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa una dakika mbili.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Ninakushukuru Mhe. Mwenyekiti.

Jengine nakuja kwenye suala la mpangilio wa tozo ambazo bado zinatumika kisheria kwa mambo ya asili. Tatizo linalojitokeza mawili tunafanya sisi katika kumbana mtu unaweza kumbana hata si haki yake kumbana, lakini kwa sababu umeambiwa umtoze pesa, utambana yule mtu wala si haki yake. Lakini kuna kipengele tu wewe utakachokibana kwamba lazima alipe. Sasa ningeomba Mheshimiwa tuyaangalie sana haya masuala ya mambo ya tozo na ada.

Sasa ningetaka Mheshimiwa tuangalie sana haya mambo ya tozo na ada. Tozo anaweza kutoleshwa mara mbili mara tatu, tozo unaweza ukambana kwa sheria. Sasa ningeshauri katika masuala ambayo tozo zetu tunapotaka kuzitoza kwa watu au masuala mengine. Halafu jengine usumbufu mtu anapotaka kuleta pesa au anapotaka kufanya kitu usimsumbue, pesa yake halafu umsumbue, anakuja kulipa kodi halafu umsumbue, anakuja kutoa tozo halafu unamsumbua. Kwa hivyo ningeomba sana Mheshimiwa katika sheria zetu tunazotunga basi zikawa ni wepesi wa kulipa, wepesi wa kumuwekea mazingira laini ili ile tozo aweze kuilipa kwa urahisi kuliko kuweza kufanya lile jambo ikawa unafanya kama unamtia adabu.

Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi naunga mkono hoja (*Makofi*)
Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Suleiman Sarahan Said. Sasa naomba nimuite Mhe. Ali Salum Haji, atafutiwa na Mhe. Ame Haji Ali na Mhe. Miraji Khamis Mussa ajitayarishe.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nikushukuru kwa dhati kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia ripoti hii ya Kamati ya Kudumu ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndigo ya Baraza la Wawakilishi.

Kabla sijaanza na lolote Mhe. Mwenyekiti, nichukue fursa hii adhimu kumpongeza Mhe. Mwenyekiti kwa namna ya uwasilishaji mzuri wa ripoti yake, ripoti ukiangalia utaona ni ndogo sana tofauti na ripoti nyengine za kawaida. Lakini imetayarishwa kwa umahiri na kama tunavyofahamu kwamba kamati hii ndio kamati ambayo imeanza kwa mara ya kwanza katika Baraza hili, nimpongeze yeye pamoja na Wajumbe wake Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo za dhati mimi nilikuwa na machache tu ambayo nilikuwa nataka kuchangia na nimeamua kuchangia hili kutokana uzito wa uhalisia wa jambo lenyewe. Jambo lililokuja mbele yetu ni jambo la Sheria na Kanuni. Sote tunafahamu kwamba ni mambo ambayo ya msingi na ya muhimu kwa kila mwanadamu. Kila mwanadamu mambo ya kisheria yatamgusa kwa namna moja au nyengine na kwa wakati wote. Sasa ni jambo ambalo ukiliangalia linahitaji uhalisia uliokuwa mzuri sana. Nishukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kwamba nchi yetu imekuwa na sheria nyingi sana, inajitahidi kila jambo kulitungia sheria ili wananchi wake waweze kuishi katika hali inayostahiki kwa kufuata mwenendo wa kisheria katika nyanja mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, lakini tatizo linalotupa mashaka sana ni Kanuni, tunatunga sheria lakini tatizo linabakia kwenye Kanuni. Kanuni zinakuwa zinachelewa sana kupita kiasi na sheria bila ya kanuni haiwezi kusimama kwa sababu kanuni ndio inayotoa ufafanuzi wa ile sheria namna inavyoelekeza. Na hili sio kama tunalizungumza kwa sababu tunapiga makelele tu, tunazungumza *as evidence* Mhe. Mwenyekiti. Mimi nataka nitolee mfano wa sheria moja tu hapa tulipitisha hapa Sheria ya Mirathi ya mwaka 2007, lakini Kanuni ya Sheria hii ya Mirathi imetungwa mwaka 2016. Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia kwa haraka haraka *within nine years* watu wana-*survive* na Sheria ya Mirathi bila ya kuwa na Kanuni na suala la mirathi tunalifahamu ni suala ambalo linatokana na maadili na misingi ya Dini zetu. Sasa unapokuwa huna jambo la Kikanuni inakuwa ni jambo la hatari, ama tutadhulumu, ama tutadhulumiwa.

Sasa niiombe basi kamati hii pamoja na Mwenyekiti, na niliombe Baraza letu tukufu hili Mhe. Mwenyekiti, kuandaa utaratibu utakaokuwa mzuri na ikiwezekana hata tutunge sheria katika sheria ndogo ndogo, kwamba tulazimishe sheria yoyote itakayopitishwa basi angalau iwe na *limit time*, kama baada ya mwaka mmoja sheria baada ya kupitishwa basi na kanuni iwe imeshatungwa, kwa sababu tusipoweka hii Mawaziri wanakuwa wanachukua muda mrefu wanajisahau. Sasa sisi kazi yetu kila siku tunatunga sheria na Sheria ukiiwacha leo keshokutwa inakuja nyengine. Hii ni athari moja kubwa sana na nazungumzia hivyo Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu si mambo yote tunayofanya sisi yametokana na Mwenyezi Mungu yote tunayofanya sisi.

Mhe. Mwenyekiti, hata ukiangalia watu wa sayansi wanayoyafanya yote yametokana na Mwenyezi Mungu. Leo tunapanda ndege hapa lakini ukiliangalia ndege, muangalie ndege mwenyewe. Ndege anavyoruka ndio anavyojua kukunja mabawa ndio anavyojua kukunja miguu na hali yake uhalisia ulivyo hasa ndio ndege ilivyo. Sasa hata hizi sheria zetu Mwenyezi Mungu ndiye aliyetuongoza kwa imani zetu ama Wakristo ama Waislam, na sisi ndio tukafuata hiyo miongozo ya Mwenyezi Mungu wetu. Kwa mfano kwa upande wetu sisi Waislam tuna Qur-ani, Qur-ani sisi ndio kama sheria yetu, baada ya Qur-ani tumeletewa na hadithi, hadithi ndio kanuni Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nitoe mfano mmoja tu katika hayo ambayo maelekezo yametuelekeza. Kwa mfano katika Qur-ani Mhe. Mwenyekiti, kuna aya inayosema, "Wa aqimus salatah wa…" Maana yake sisi Waislam na Wakristo kwa upande wao na kwaa imani zao tuna ulazima au tuna wajibu wa kusimamisha sala. Lakini Qur-ani haikutoa ufafanuzi wa sala, iliyotoa ufafanuzi wa sala ni hadithi, hadithi ndio inaelekeza namna gani ya hiyo sala kusaliwa, namna gani kabla ya kusali uwe, maana yake unatakiwa utie tohara utie na udhu, lakini hadithi ndio inayoelekeza ukitaka kusali uelekee wapi, baada ya kuelekea Kusini ma Mashariki, uelekee Kaskazini. Lakini pia hadithi hizo hizo ndio zinazotuelekeza utaratibu wote wa hiyo sala. Sasa maana yake nini kusema hivi, ndio nakazia pale pale kwamba sheria bila ya kanuni inaweza ikatupelekesha katika pahala pasipostahiki na kuwakosesha watu haki zao za msingi kwa kutoa maelekezo yaliyokuwa sahihi.(*Makofi*).

Chengine Mhe. Mwenyekiti, nataka nizungumzie ushirikishwaji wa wadau. Hizi sheria na kanuni vina watu vinawagusa na ndio tunaojitungia kwa sababu na sisi ni sehemu ya wadau, sehemu ya wananchi. Sasa ningeomba nimeona katika kitabu chao na wamezungumza katika ukurasa wa kumi na mbili na kumi na tatu, ushirikishaji mdogo wa wadau, unapokosa kuwashirikisha wadau katika hali ipasavyo, kuna athari ndani yake. Hata karika ripoti yao pia wamejaribu kuzungumza kwa sababu tunaweza kufika pahala tukaweza kutunga sheria, tukatunga kanuni zinazopelekea muingiliano baina ya taasisi na taasisi au eneo na eneo. Matokeo yake ikajakuwa kuna *conflict* ndani yake. Sasa ni vyema niombe tu kwamba tunavyoandaa mambo haya basi ni vyema tukawashirikisha wadau ipasavyo.

Lakini la mwisho Mhe. Mwenyekiti, mwenzangu alizungumzia lakini na mimi nazungumzia kwa upande wangu suala la uandishi wa vitabu vyetu hivi vya kanuni na sheria, kwamba katika ripoti yao hii wameelezea kwamba kuna athari zinazotokezea za kimaandishi. Sasa mimi niombe tu ushirikiano baina ya taasisi ambazo zinapeleka kanuni zao ama sheria zao kuandikwa pamoja na taasisi yetu ya Wakala wa Upigaji Chapa ya Zanzibar, kuwa na ushirikiano maalum katika kutengeneza vile vitabu ili kuja kuondoa hizo istofahamu za

kasoro mbali mbali katika vifungu vinavyoandikwa katika kanuni zetu ili visije vikaleta athari baadae katika matumizi.

Mhe. Mwenyekiti, nilisema tu kitabu kidogo lakini ufafanuzi wake ni mkubwa na una upeo mkubwa sana. Mimi sitopenda kwenda *deep* zaidi na natoa fursa hii kwa wenzangu wapate nafasi ya kuweza kuchangia kwa kina, kwa sababu jambo la sheria ni jambo zito ni jambo ambalo linamgusa kila mtu na kanuni kama tunavyozungumza. Sasa niseme kwamba fursa ndio hii ndio yetu sisi katika kukalia suala hili.

Lakini kabla sijamalizia Mhe. Mwenyekiti, nimeletewa hapa kimemo cha Kiswahili fasaha na mwalimu wangu, nimezungumza lugha ya wadau, lugha tafsiri sahihi tunaambiwa ni wahusika sio wadau. Kwa hivyo naomba niweke *Hansard* sawa Mhe. Mwenyekiti, baada ya neno wadau tuzungumze neno wahusika.(*Makofi*).

Baada ya kusema hayo na mimi kwa niaba yangu na wananchi wangu wa jimbo la Kwahani naunga mkono hoja ya hotuba ya ripoti ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ahsanteni. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Ali Salum Haji Mwakilishi wa Kwahani. Sasa naomba nimuite Mhe. Ame Haji Ali, atafuatiwa na Mhe. Miraji Khamis na Mhe. Panya Ali Abdalla ajiandae.

Mhe. Ame Haji Ali: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa fursa hii ndogo na mimi niichangie, kwa kuwa ni mjumbe wa hii kamati basi kuna baadhi ya maeneo ambayo nimeona bora basi tuyakazie kazie kidogo baada ya ripoti yetu. Kwanza naomba kwa ruhusa yako naomba nichukue fursa hii kumshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati yetu kwa uwasilishaji wake mzuri mahiri ambao umependezesha humu Barazani.(*Makofi*).

Lakini nikianza katika mchango wangu kama kitabu chetu kinavyoeleza pale mwanzo katika utangulizi, kamati hii ina majukumu makubwa sana. Hii kamati ina majukumu makubwa kama yalivyotajwa pale katika ukurasa wa mwanzo, kwa hivyo ni vizuri sasa tukaipa nafasi ikafanya kazi zake kama vile ambavyo imepangiwa.

Lakini la pili Mhe. Mwenyekiti, wakati tulipofanya ziara katika maeneo mbali mbali na kamati tulijifunza mambo mengi katika utendaji kazi wetu. Kama Mhe. Mwenyekiti alivyoonyesha katika kitabu chetu hichi ukurasa wa nne na watano, tumefanya ziara mbali mbali kwa Mhe. Mwanasheria Mkuu na taasisi

nyengine, tukajifunza mambo mengi ambayo mimi kwa niaba ya kamati tu naiomba taasisi husika iyasimamie yale mambo kama vile ambavyo tumeyaelekeza.

Lakini jengine pia katika hapo hapo tumeambiwa tusitumie neno wadatu, tutumie neno wahusika. Tumeona katika maeneo mengi tuliyokwenda katika ziara zetu na zile taasisi ambazo zinahusika na utungaji wa Kanuni, basi bado tunahimiza sana kwa wale wahusika kushirikishwa. Kwa sababu Kanuni hizi na taratibu hizi tunawapangia watu kule, sasa tusivyowashirikisha ipasavyo, huenda ikawa matumizi sasa yatakapokwenda kwao ikenda kuwa ni vikwazo. Kwa hivyo tunahimiza sana sisi kwa mujibu wa tulivyoona katika kufuatilia yetu ni kwamba ushirikishaji wa hao wahusika ni mdogo sana katika utungwaji wa kanuni zetu hizi, basi tunaziomba zile taasisi husika zinapoanza mchakato huu basi wawashirikishe wahusika vile ipasavyo.

Pia katika kuendelea naiomba sana tuna maoni mengi pale tumetoa katika kitabu chetu pale ukurasa wa kumi na sita na kumi na saba, wahusika wote wayatizame yale ili hizi kazi zetu ziweze kwenda vizuri, kama ustadhi aliyemaliza kusema pale hizi Kanuni tukizifuatilia basi zitaleta mwanga mzuri zaidi.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine ambalo nalo tulilisema kwa msisitizo kidogo ni kwamba bado kamati yetu inakwazwa na kile kifungu cha Kanuni ya Baraza hili ya 33 *section* ya nne. Mimi naomba sasa tuchukue nafasi ya kukirekebisha hiki kifungu ili tuweze kuipa nafasi kamati ifanye kazi zake vizuri kwa niaba ya Baraza kama ulivyo utaratibu wa mambo mengine.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi kwa sababu nimesema ni Mjumbe wa hii kamati sitaki kuchangia sana kwa sababu haya yote ambayo tumeyaandika nilikuwa nimeshiriki, lakini nimalizie tu kwa kusema kwamba, katika ukurasa ule wa ishirini na moja na ishirini na mbili katika kitabu chetu tumetoa maoni na mapendekezo mengi sana mle. Kwa hivyo naziomba taasisi husika zote zijaribu kuyachukua haya maoni na mapendekezo yetu kwa mustakabali wa uboreshaji wa kamati yetu na mustakabali mzima wa utendaji wa kazi zetu.

Baada ya kusema haya mafupi mimi kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wote wa jimbo langu naunga mkono kitabu hichi kwa asilimia mia moja.

Ahsante Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Ame Haji Ali kwa mchango wako. Sasa naomba nimuite Mhe. Miraji Khamis Mussa na atafuatiliwa na Mhe. Panya Ali Abdalla na Mhe. Suleiman Makame Ali ajiandae.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuchangia ripoti hii ya kamati ya Sheria ndogo ndogo. Kwanza Mhe. Mwenyekiti, naomba sana nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati kwa uwasilishaji wake lakini pia na ripoti aliyotupa imeenda vizuri sana hasa kwa kuwa Kamati hii ni mpya, hawakuwa na *reference* pahala, *reference* ni wao wenyewe na Wajumbe wake wa Kamati na baadhi tu ya vianzio ambavyo walikwenda kuvifanyia kazi. Lakini nimpongeze zaidi Mwenyekiti alipokuwa anawasilisha Makamo Mwenyekiti wake ndio alikuwa anasimamia yale aliyokuwa anawasilisha, kwenye hili amepata bahati kubwa sana mambo mawili kwa wakati mmoja.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo naomba niende katika muhtasari wa Mwenyekiti aliyekuwa anawasilisha, nilikuwa namsikiliza kwa makini. Katika jambo moja alilolizungumzia na ni muhimu sana ni suala la mafunzo kwa kamati hii lakini pia suala la mafunzo kwa *secretariat* ya kamati. Mimi niunge mkono kwa asilimia mia moja, kuna haja ya kufanyiwa mafunzo haya lakini kuna haja pia ya kupewa ziara tofauti ambazo zitawajengea uwezo kamati hii. Kwa sababu kwanza upya wao, lakini la pili wao wenyewe wana sehemu ya majukumu kwenye kamati nyengine. Sasa kuwepo kwenye kamati hii sasa wasipopata mafunzo wanaweza wakayabeba ya kule ambayo hayafanani na huku. Sasa kuna muda wakitengewa, wakipewa mafunzo, wakiwezeshwa katika ziara tofauti, naamini kitabu hichi kitakuja na sura nzuri zaidi ya hapa ambavyo wamefanya. Kwa hivyo kwenye jambo hili la kuwapa uwezo mimi naungana nalo asilimia mia moja kama nitakavyoungana katika hoja hii ya kamati huko mbele.(*Makofi*).

Lakini la pili walidai suala zima la marekebisho ya kifungu cha 33(4), ni kweli unajua mimi naamini tulipokuwa tunapitisha Kanuni hii tulijua kuwa Wajumbe watakaotokana na kamati hii ni Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ambao watakuwa kama ni sehemu ya kamati ya kudumu. Lakini Wajumbe tulivyowapata ni Wajumbe ambao wanatokana na kamati nyengine. Kwa hivyo wana majukumu kwanza katika kamati zao, lakini wana jukumu la pili la kuja kufanya kazi kwenye kamati hii. Kwa hivyo ukiwapa miezi mitatu, inawezekana mwezi mmoja kwa sababu sehemu kubwa pia ya Wajumbe hawa ninao mimi Kamati ya *PAC*, tukienda wiki tatu, maana yake tumeshaua mwezi. Sasa leo ukimpa miezi mitatu imeshawasilishwa hapa na Kanuni hizi zimekuja zaidi ya tatu; moja, mbili, tatu, hawawezi kupata muda ukakidhi yale matakwa ya kifungu hichi. (*Makofi*).

Sasa niungane nao mkono ingekuwa Wajumbe hawa moja kwa moja wamepatikana hawana kamati nyengine wanazozifanyia kazi basi miezi mitatu hii ingekidhi, lakini hoja ni kwamba wanatumika katika maeneo yao na yawezekana katika zile kamati zao kuwa *PAC* wako Pemba, lakini Ustawi wa Jamii wako Matemwe. Sasa kuwakusanyisha na wakaacha majukumu katika kamati zile ni mtihani pia. Sasa mimi ningependekeza tu hili tulibebe lakini lije katika sura ya kulirekebisha baada ya mitatu, basi tuwape miezi sita. Ni jambo la kawaida ambalo hatukuliona mwanzo, sasa hili tulizingatie katika kuboresha utekelezaji wa kamati. Haya ndio ambayo niliyaona katika ripoti ya moja kwa moja ya mwenyekiti lakini na haya aliyotupa Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende katika Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar. Katika eneo hili kuna makosa hapa ambayo yameripotiwa katika Wakala wa Uchapaji, lakini kazi ya uchapishaji ni kazi pia inahitaji umahiri wake. Ningeshauri Wakala yule pia tukampa wahariri ambao watapitia zile *documents* za kisheria, kwa sababu yawezekana tunao watu ambao wanakwenda kuhariri yale machapisho yetu. Lakini tunavyopeleka Miswada, Miswada hii inakuwa katika lugha za kisheria, basi ningependa kuwaambia wenzetu wa Serikali, wakaandaa wahariri mahususi watakaokuwa wanazipitia zile *documents* za kisheria ambazo zinakwenda katika Wakala wetu wa Uchapaji, tunaweza tukaboresha hiki kituna ikaja hapa yale makosa ambayo wakati mwengine unatizama kifungu cha Mswada wa Kiswahili na wa Kiingereza yanapishana. Sasa kikubwa zaidi kinaonekana hakuna wahariri ambao wanaweza wakatusaidia katika kuweka sawa Miswada yetu tunayoichapisha, hasa ile inayokwenda kwa taratibu za kisheria zaidi.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti naomba niende ukurasa wa tisa kuna maeneo hapo yamezungumzwa ada na tozo zipewe mazingatio katika mahitaji kwa yale maeneo husika. Nilivyofahamu mimi kama ni sahihi Mhe. Mwenyekiti, kuwa tunapitisha tozo mbali mbali hasa katika hizi Serikali za Mitaa, yawezekana tozo ile kama kama tunaipitisha katika utaratibu ya umoja, inatakiwa itumike katika Manispaa ya Mjini, inatakiwa itumike katika Manispaa ya Magharibi "A" lakini pia katika Halmashauri zetu. Kwa kuwa Kanuni hii kuna Mabaraza mle ni vyema wanapotunga Kanuni basi yale mazingira yakae katika *local government* tuwe tunayazingatia. Kwa sababu tozo ambayo unaweza ukampa mtu, tunayempa huduma mjini tofauti na mtu ambaye tunampa huduma Mahonda. Sasa mazingira yale wameyazungumza Kamati hapa kulingana na eneo la tozo ambalo lipo ukurasa wa 9. Nilikuwa napendekeza hizi tozo tuzipitishe kulingana na mazingira ya maeneo yenyewe.

Ukurasa wa 17 nakwenda na mimi kuungana na Mwalimu Ali Salum Haji (Kirova), alitoa hadithi ya kuwa tusimamishe sala na tutowe zaka, lakini yeye kazungumza kwa ufupi tu. Lakini katika muhtasari hasa tumeona mapungufu

ya uwepo wa Kanuni. Kuna eneo moja la jaduweli hapa la kitabu hichi linasema Kanuni zinatayarishwa. Lakini jaduweli jengine linasema rasimu ya Kanuni imeshakamilika. Lakini jaduweli jengine pia nalo Kanuni zake hazijatungwa kutokana na kwamba Sheria za Kamisheni za kuanzisha Afisi ya Mufti ya Zanzibar Nam. 9 ya mwaka 2001 zinafanyiwa marekebisho kwa pamoja.

Mhe. Mwenyekiti, utayakuta maeneo haya yote yamekosa Kanuni, Sheria imetungwa lakini imekosa Kanuni, sasa ni muda mrefu. Hata kama hapa kuna kisingizio kuonekana kwa sheria hii ya 2001 ilikuwa ina kasoro, inawezekana mapungufu yale, tungekwenda kutungwa Kanuni, tungeweza kuelezea yale mambo ambayo kasoro zake na uchambuzi wake tukazipata katika eneo hili, lakini kuwa leo rasimu ya kwanza ya Kanuni imeshakamilika tokea 2007.

Mhe. Mwenyekiti, wakati mwengine tunaweza tukapitisha rasimu lakini katika utekelezaji wetu ikawa rasimu nyengine sio kipaumbele chetu. Lakini katika utekelezaji huu ni mtihani. Nimuombe tu Mhe. Waziri anayehusika na masuala haya ajitahidi sana katika yale yale aliyoyazungumza Shekhe Ali Salum Haji (Kirova), kuwa tufike pahali tuzingatie yale maslahi ya watu kutoka katika maeneo ya zakka lakini kutoka katika maeneo mengine ambayo yamezungumzwa hapa kama ambavyo wenzangu wamesema. Najua Waziri mahiri, ana uwezo mkubwa basi tu atusaidia kukamilisha ili ile mivutano ya kisheria iwepo. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende ukurasa wa 20. Wenzetu wa Kamati hapa wamezungumzia kutumika kwa lugha za kigeni hasa katika majaduweli mengine tunayaona. Jaduweli la Wakfu huku mwanzo kuna Kiswahili kizuri lakini mbele ndani yake kuna Kiingereza. Eneo moja linalotoa tafsiri ya mtu kupata huduma mwanzo anapata kwa Kiswahili, ukurasa wa pili anapata kwa Kiingereza, yaani ni vitu ambavyo vinasikitisha sana. Sasa tuone lugha yetu tunayoitumia kama ambavyo wana kamati wameelezea, basi lugha yetu tuitumia ili tuache kutoa machapisho kwenye lugha za kigeni hasa katika machapisho yale ambayo wananchi wetu wanakwenda kupata huduma.

Mhe. Mwenyekiti, eneo la mwisho ukurasa wa 21 utungaji wa Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo kwa Mawizara na Tasisi zake. Lakini kifungu ambacho nataka kuungana na Kamati ni kifungu Nam.(c) ikiwezekana Kanuni ya Baraza itoe uwezo wa Kamati, iwe na uwezo wa kupitia na kuzichambua Kanuni na Sheria ndogo ndogo zilizotungwa miaka ya nyuma.

Mimi nikubaliane na wana kamati kuhusu eneo hili hasa ukizingatia, kama leo tumezungumza kuna sheria zimetungwa mwaka 2007, lakini Kanuni zake mpaka leo hazipo ndio kwanza zipo kwenye rasimu zinarasimishwa,

inawezekana kurasimishwa kwengine pia kapewe mtu mwengine siye Waziri anayehusika na hii Wizara. Eneo hili tukiwapa mamlaka ya kupitia zile Kanuni ambazo sheria za huko nyuma wenzetu hawajazipitia, lakini pia zimetungwa na zipo lakini waweze kuzipitia kama ipo haja. Naungana nao mkono kwa sababu yapo mapungufu wanaweza wakashauri, lakini yapo mafanikio pia wanaweza wakatupa taarifa zikaweza kutusaidia katika uwepo wa sheria zetu.

Naomba Mhe. Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumpongeza tena Mhe. Mwenyekiti, kwa uwasilishaji wake, niwapongeze wana kamati wote lakini kwenye eneo hili naomba sana kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na kuwaomba wale viongozi wanaohusika na Kanuni zilizokuwa bado basi muungane na Kamati waendelee kuipa msaada Kamati, ili kuziwezesha Kanuni zile zimalize na kufanya kazi kwa wakati unaohusika ili kuweza kuwasaidia wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru. (Makofi).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Miraji Khamis Mussa kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Panya Ali Abdalla atafuatiwa na Mhe. Suleiman Makame Ali na Mhe. Waziri Said Soud Said ajiandae.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujaalia uhai tukaweza kukutana hapa katika Baraza letu hili Tukufu. Pia nichukue fursa hii kukushukuru wewe na mimi kunipa fursa niweze kusema machache katika Kamati hii.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza sana Mwenyekiti, wa Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo kwa uwasilishaji wake mzuri kabisa ambao umeonyesha umahiri na uweledi wake katika kazi hii. Pia nichukue fursa hii kulipongeza kwa dhati kabisa Baraza letu Tukufu kwa kuona umuhimu wa kuiunda Kamati hii ya Kanuni na Sheria ndogo ndogo, kwa kuona jinsi gani tunaweza Kamati hii ikapata fursa ya kuzipitia Sheria zetu na Kanuni, ili tukaona penye mapungufu tukaweza kuparekebisha. Mheshimiwa ni pongezi kubwa sana kwa Baraza kuona umuhimu wa kuwepo Kamati hii.

Mhe. Mwenyekiti, uwepo wa Kamati hii na kwa kuwa Kamati imeanza kuundwa sio muda mwingi na Mwenyekiti wakati wa usailishaji wake alieleza juu ya umuhimu wa kupatiwa elimu ni suala la kuzingatiwa sana. Kwanza kuona Kamati yenyewe ni mara yake ya mwanzo kuwepo katika Baraza letu, lakini na kazi yake ilivyokuwa inahitaji uwelewa mpana. Kwa hivyo suala la elimu ni suala ambalo lisiwe na kigugumizi lazima hawa wapatiwe elimu ili waweze kufanya kazi zao vizuri inavyotakiwa.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, wenzangu wengi wameeleza na mimi naweka msisitizo. Umuhimu wa kuweka Kamati hii na kuwepo na Kanuni ya kifungu 33(4) ambacho kimo katika Kanuni zetu za Baraza, naomba sana tuzingatie kuweza kufanyia marekebisho Kanuni hii ili iweze kuwapa fursa nzuri ya utendaji wa majukumu ya kazi zao. Kazi za kupitia Kamati na Kanuni ni kazi ngumu na zinahitaji muda wa kutosha, ili kile tunachokipitia basi tuweze kukifanyia kazi kwa usahihi. Ni masikitiko wakati imeletwa Kanuni ya makampuni na ni suala muhimu sana kwa jamii kuwa imeletwa wakati mumo katika kazi za Baraza, hamkuweza kufanya kazi kama inavyopaswa. Hii haitaleta mafanikio mazuri katika utendaji wetu. Ni vyema Kamati ipangiwe muda maalum iweze kupitia Kanuni au Sheria zenye mapungufu ili kile kinachojadiliwa kiweze kupatikana usahihi wake.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, Kamati hizi zimetueleza jinsi ya mapungufu ambayo wao wamebahatika kuyaona na mimi nataka niungane nao na nikubaliane nao hasa katika Kamati Kanuni za mirathi ya Kiislamu. Kama tunavyoelewa mambo ya mirathi ni mambo yenye migogoro sana katika familia zetu, kukosekana Kanuni ambayo inaweza kuichambua sheria ile ikaweza kuirahisishia kazi ni tatizo. Mhe. Mwenyekiti, imeelezwa kwamba sheria hii imetungwa tangu mwaka 2007 ni jambo la masikitiko kama mpaka muda huu Kanuni yake haijapatikana. Lakini pia yamejitokeza masuala mazima ambayo sisi wenyewe ni mashahidi tunayaona kila wakati unapofika wakati wa Hijja. Ni kweli kungekuwa Kanuni zipo na utaratibu mzuri ukapangwa, yasingeweza kujitokeza masuala kama yale tunayoyaona wananchi wetu wanadhulumiwa pesa zao, halafu hawapati kushiriki katika ibada ile tukufu.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana tuzingatie utungaji wa Kanuni, kwa sababu hili la kwenda Hijja wananchi wanapokosa fursa vizuri, wanapokosa kuandaliwa maandalizi yao vizuri, tunaweza tukasababisha kuwakatisha tamaa watu ambao tayari wana muelekeo wa kutaka kwenda Hijja, wakaona kumbe wao hakuna chombo kinachowaratibu vizuri shughuli zao, wanaweza wakawa hawaviamini vile vikundi moja kwa moja kwa sababu havina utaratibu mzuri. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, ili tuwe na utaratibu mzuri lazima tuandae Kanuni ili Kanuni hizo zitamtaka kila mmoja aweze kuyatumia matakwa ya Sheria yaliyokuwepo pale yanayomtaka yeye katika usimamizi wa vikundi vile, na hapo tutafanikiwa tutapeleka Mahujaji wetu vizuri na tutaweza kushughulikia mambo ya mirathi vizuri lakini pia tutaweza kushughulikia hizi Zakka na Sadaka. Pengine hatuzipati haziji kwa sababu hazipo katika utaratibu mzuri, kwa hivyo waletaji wanahisi hawaoni wakipeleka zakka zao na sadaka zao vipi zitaweza kuwafikia walengwa wale wanaokusudiwa katika kupewa hizo Zakka na Sadaka.

Mhe. Mwenyekiti, pia Kamati hii imeeleza changamoto na mimi nataka nizirudie hizi changamoto ambazo wamezisema ili tuzione umuhimu wake. Kwanza walisema msisitizo uliotolewa kwamba ni vyema kabla ya kutunga Kanuni na Sheria ufanywe utafiti wa kina wa utakaopelekea ufahamu mahitaji halisi ya jamii husika. Ni kweli kukifanyika utafiti ndipo tutaweza kuziandaa Kanuni ambazo zitaendana sambamba na jamii yetu, hili ni suala muhimu sana.

Pia kuna changamoto ambayo imeonesha kwamba kuna umuhimu wa watunga sera, sheria na kanuni washirikiane katika hatua zote zinazostahiki, ili kuepuka kuwepo kwa mawazo tofauti. Mhe. Mwenyekiti, ni kweli hili lipo, sheria hizi ambazo tunazo tayari zipo nyengine zinagongana na sera. Kwa hivyo kuchukua hatua ya kukaa pamoja kutaweza kuona kila mmoja kile anachokipitisha basi hakigongani na mwenzake na hatimaye hatugongani hata na sheria kuu, ni vizuri sana.

Pia wameeleza changamoto nyengine ambayo kuitaka Wizara au Taasisi za serikali zishirikiane wakati wa kutunga sera, sheria na kanuni kwa ajili ya kuepuka migongano isiyo na lazima. Mhe. Mwenyekiti, ni kweli huu ushirikiano kwa sababu tunaona kuna sheria nyengine katika taasisi hasa kama hizi sheria zenye makosa na adhabu, utakuta adhabu huku imesemwa vyengine na katika taasisi nyengine imesemwa vyengine. Kwa hivyo mkiweza kukaa pamoja kushirikiana mtaweza kuiweka vizuri sheria hiyo na ikaweza kutumika vizuri kwa jamii.

Mhe. Mwenyekiti, wenzangu wameeleza sana katika makosa ya uwandishi au lugha isiyokuwa fasaha au lugha ngumu katika sheria hicho kinakuwa ni kikwazo kwa jamii kutokuielewa sheria yao imekusudia jambo gani. Ni muhimu sana kuweza kuwa na lugha iliyokuwa rahisi ili wananchi wetu waweze kufahamu sheria zinawaeleza nini na wao waweze kufuata sheria za nchi yao.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sina mengi ya kusema isipokuwa msisitizo wangu nisisitizo tu serikali kuona umuhimu wa utungaji wa Kanuni ili sheria zetu ziweze kuwa na utekelezaji ulio sahihi, ili kuepusha ile migongano iliyokuwa haina ulazima. Muda mwingi hapa tulikuwa tunasema jamani kile kifungu kinachomtaka Waziri atunge Kanuni kinasema "Waziri anaweza akatunga Kanuni", Sasa hii kuiweka anaweza ndiyo maana wengine imewafanya wa-*delay*, waone kwamba hakuna umuhimu naweza nikatunga, naweza nisitunge. Kwa hivyo ikawa hakuna jambo la uzito. Mimi bado naiomba serikali kuweka msisitizo kwamba lazima sheria ikishapitishwa lazima Kanuni itungwe ili iweze kutoa urahisi wa kuitekeleza sheria hiyo.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, naungana na Wajumbe wenzangu wote waliochangia na nawaomba wengine waichangia kwa umuhimu mkubwa wa kuwepo Kamati hii, tuichangie ili iweze kufanya kazi zake kiusahihi.

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono kwa asilimia mia moja.(Makofi).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru kwa Mhe. Panya Ali Abdalla kwa kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Suleiman Makame Ali atafuatiwa na Mhe. Waziri Said Soud Said na kabla ya kumwita Mwenyekiti nitawapa nafasi Mawaziri husika kama wana chochote katika hoja hii.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia ripoti hii ya Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo za Baraza la Wawakilishi. Wengi wamesema hapa na ndiyo ilivyo kwamba Kanuni inaendana na Sheria.

Mhe. Mwenyekiti, hapo niende kwenye kuwapongeza kwanza Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hii hususan Mwenyekiti, mahiri Mhe. Rashid Makame Shamsi kwa kuhakikisha wametuletea kitu ambacho hawakuficha kitu. Niwapongeze sana na Inshallah nawatakia kila la kheri ili kuhakikisha tunafanya kazi ya kujenga taifa.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo niende kwenye ukurasa wa 7 kwenye suala la Mkutano wa wahusika. Maana Mhe. Haroun Ali Suleiman (Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora) anasema kwamba sio wadau ni wahusika Kiswahili fasaha.

Mhe. Mwenyekiti, niende moja kwa moja kwenye Mabaraza ya Manispaa na Miji, niwapongeze sana Mabaraza haya kwa kuhakikisha wanaturudishia nidhamu kwenye miji yetu ili kuwa masuala ya usafi na mipango mengine, ili kuhakikisha kuwa miji inatembeleka wakati wote. Kuna kitu ambacho Mabaraza haya au Manispaa zetu hizi, hususan nimegundua kwa hapa Mjini Unguja, Mhe. Waziri ningeomba vizuri zaidi angenisikiliza kwamba kuna tatizo kubwa la wale vijana au askari wetu wamewekwa pale kuhakikisha miji yetu inakuwa safi. Mhe. Mwenyekiti, lakini chakusikitisha askari wale wanapita katika maduka yaliyokuwepo ndani kule Vikokotoni na sehemu nyengine na kuanza kuwaonea onea wale wafanyabiashara hufika mpaka wakati mwengine wakachukua ngua au bidhaa zilizokuwemo katika yale maduka na kuwasumbua au kuwatoza faini wakati wanakuwa wapo kisheria.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilitaka nijue hapa ipo Kanuni inayosema hivyo, kwamba kutokufuata ile Kanuni iliyowekwa kwamba ukiweka hapa tunakuondosha, lakini wakati mwengine wanakwenda madukani wanachukua

vile vitu, kusema la ukweli ni kuwaonea. Sifikirii kama ipo Kanuni hiyo. Siku moja nilipata kuwauliza walikuwa hawajui kama mimi ni Mwakilishi, nikawauliza hapa alichokifanya huyu ni kosa, wakasema si kosa, nikawauliza sasa kwa nini mkafanya. Naomba sana Mhe. Waziri alichukue hili kuhakikisha kwamba anasema nao watu wake, na wale ni wafanyabiashara, serikali inapata faida kutoka kwao. Kanuni hizo kama zipo basi ziangaliwe vizuri na kama hazipo basi wapewe utaratibu wa kufahamishwa wale.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende moja kwa moja kwenye masuala ya kusimamia Kanuni za mirathi, hususan kwenye masuala ya wakfu. Hapa mara nyingi panatokea migongano, baadhi ya siku nyengine kunakuwa Wakfu zile mali wanazo wao lakini inatokea taasisi nyengine wanataka kuimiliki wao. Sasa hapa inakuwa mgongano kidogo wa Kikanuni na utaratibu ili kuweza kujua zile mali ni ya Wakfu au ni mali ya nani, kwa sababu mara nyingi inapotokezea hivi huwa mambo haya ya mirathi na mambo mengine yanapata kusumbuka sumbuka.

Mhe. Mwenyekiti, hata Mhe. Bi Panya Ali Abdalla alisema kwamba masuala haya ya mirathi ni mambo ya kuangaliwa. Ni kweli kuna baadhi ya wakati wengine wale wanaostahiki kurithi zile mali wanakoseshwa, kwa sababu ya kifedha ya yule mtu mwengine ama kwa sababu ya nyengine yeyote ile. Ni vizuri sana kuangalia hizi Kanuni na taratibu pamoja na kuendana vizuri na sheria zilizopo ili kuhakikisha wale wanaohusika basi zile mali wazipate kama ilivyo.

Mhe. Mwenyekiti, lakini nikitoka hapo niende moja kwa moja hata kwenye hizi Kanuni zetu siye za Baraza la Wawakilishi Mhe. Mwenyekiti, wakati mwengine hukaa nikaumiza kichwa kama sasa hivi hapa tunaripoti tunazisubiri mwezi wa tisa. Ripoti mwezi wa tisa za maagizo ya kamati, siku nyengine kile kitu hakijafanyika kwenye yale maagizo lakini tunapitisha bajeti tunasubiri mwezi wa tisa ambapo bajeti nyengine imeshapita.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti na hili nilikuwa nikuomba kwamba lifanyiwe marekebisho liangaliwe vizuri kwamba ripoti tunaisubiri mwezi wa tisa tunakuja kujibiwa kwa mfano inatakikana wizara itekeleze kile kitu ambacho kwamba tumekipitishia ndani ya bajeti hii 2017/2018, lakini unaona kitu kile hakifanyiki lakini bajeti yake imeshapita siku nyengine inafika mpaka 2019 inakuja kufanyika hivyo. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti mimi nilikuwa naomba sana kwamba kuangaliwa na hizi kanuni zetu tunazokwenda nazo ili kuhakikisha kwamba tunakwenda vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, yangu mimi yalikuwa ni hayo lakini naunga mkono ripoti hii asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana nakushukuru Mhe. Suleiman Makame Ali. Sasa naomba nimwite Mhe. Waziri Said Soud Said atafuatiwa na Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ ajiandae.

Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Ahasante Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, mimi nimefarijika sana niliposema hiki kitabu *page* namba 6 kwenye kifungu cha (c).

Kifungu hiki kimenifanye kidogo nifunguke na kwa nini nasema hivyo kwa sababu nimeona hapa Kamati imetembelea Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar na kuelezwa namna inavyoelekeza majukumu yake kwanza ikiwemo kufanya utafiti kabla na wakati wa kuifanyia mapitio sheria mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nataka niseme kwamba katika mazingira ya uongozi bora, nchi ambayo inaongozwa na Katiba na Sheria, basi mambo kama haya yana ulazima mkubwa sana kushughulikiwa. Ninataka nichukuwe nafasi ya kusema kwamba haya yamekuja baada ya kuwa yanaongozwa na kiongozi mahiri Dkt. Ali Mohamed Shein Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, kimsingi kuna mambo mengi yanahitaji kufanayiwa marekebisho ili wananchi wa Zanzibar waweze kupata haki zao zinazostahiki na pale yanapotokea mambo, basi vile vile lazima Wazanzibari waweze kujua mambo yale yanakwenda vipi na yanaishia vipi. Kwa vile nataka nichukuwe nafasi pekee ya kupongeza Kamati za Baraza la Wawakilishi kwamba zimefanya kazi nzuri sana ya kutafuta mambo mbali mbali na hatimaye kuisaidia Serikali ili iweze kuyaona mambo kama yale na kuyafanyia kazi.(*Makofi*).

Lakini pia ni wajibu wao kamati kuibua hata yale ambayo mambo yamejificha kwa mfano nchi hii ilizama meli ikauwa watu wengi sana kutoa Unguja na Pemba. Kamati sijaiona wapi wameandika na lazima watoe taarifa kamati, kesi hiyo ilikwenda wapi, iliishia wapi kwa sababu waliokufa si dagaa ni watu, waliokuwa na mali zao waliokuwa wanahitaji kulipiwa bima, waliokuwa mizigo yao inahitaji kulipiwa bima. Sasa kamati ilikuwa itupe taarifa na nasikia Mhe. Mwenyekiti, nasikia bado naendelea kukuambia tena, nasikia kwamba meli hii ilikuwa inamilikiwa na Bwana Jaku Hashim Ayoub, nasikia na ninaposema nasikia maana yake *hears evidence have not evidence*.

Mhe. Mwenyekiti, kamati ilikuwa inataka itowe taarifa Wazanzibari wajuwe wapi na lini kitu kile kimesimama, lakini pia nataka niipongeze Kamati pia kwa kuibua mambo madogo madogo ambayo yatatusaidia kujenga utawala bora katika nchi yetu. Kwa mfano Mhe. Mwenyekiti, kuna mambo ambayo yanafanyika na kwa kuwa hayajatungiwa sheria ndogo ndogo basi yanatukwanza. Kwa mfano mtu anakwenda kuomba leseni, anaomba leseni ya kuuza duka na anapewa leseni ya kuuza duka lakini baadaye anaweka mikakati, simuuzi huyu CCM, simuuzii lazima duka langu anunuwe CUF, akienda CCM, akienda chama chengine hauziwi.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, nakueleza haya kwa ushahidi maana mimi yamenikuta hayo, mimi hayo yamenikuta. Kwa vile sheria lazima iweke bayana ikiwa umechukua leseni ya kutoa huduma na hutaki kutowa huduma, una ubaguzi wa kutoa huduma basi sheria ichukuwe mkondo wake wa kunyang'anywa leseni, yaani kuwe na vifungu vinavyoeleza mambo kama haya.

Mhe. Mwenyekiti, unaendesha gari huwezi ukasema kwamba gari langu lazima nipakie CCM, lazima nipakie CUF, hakuna hiyo umechukua leseni ya kutoa huduma utowe huduma. Nitakupa mfano Mhe. Mwenyekti, kulikuwa na ziara ya Mhe. Ibrahim Lipumba Pemba magari yote yamezuwiwa yameanza kazi saa sita, eti asitowe huduma juzi. Yaani ni jambo la ajabu kabisa wamechukua leseni unataka kutoa huduma lakini kuna mtu anakukalia mbele anakwambia usitowe huduma, huduma hii maana yake ukiitoa basi watu watakwenda kumpokea Lipumba, *how come* itakuwaje, demokrasi hayendi hivyo.(*Makofi*).

Sheria lazima itamke waziwazi umechukua leseni ya kutoa huduma ya abiria gari yako lazima ifanye kazi kuchukua abiria na usichaguwe, halikadhalika umeomba kibali cha kuchimba kisima unasema kisima hiki CCM hateki maji hapa, lazima maji haya yatatekwa na CUF lakini CCM hathubutu kuja kuteka maji hapa. Lazima sheria itamke bayana kwamba ukifanya mambo kama hayo siku ya pili liende tani kumi la mawe likatie kisimani kifukiwe kisima kazi imekwisha, sheria iseme tusiwe na utaratibu wa kutunga sheria lakini sheria zenyewe zikawa zinachezewachezewa.

Mhe. Mwenyekiti, hali kadhalika lazima kuwe na sheria zinazowafanya watu wanoharibu bahari ziwekwe wazi na Kamati ya Baraza la Wawakilishi zifanye kazi, kuwe na sheria zinazowafanya watu wanotumia lugha mbaya kwa viongozi, unweza kwenda bandarini, unaweza kwenda pahala wewe ukawa kiongozi unajulikana lakini akatoa mtu akakukejeli kwani kiongozi huyu, kwani Mwakilishi huyu, kwani hivi, kuwe na sheria na sheria zile ziwe kama zile sheria zinazozungumzia madereva wanaopigwa faini papo kwa papo, yaani akikuchukua tu akikupeka kituoni kuna ushahidi amemdhalilisha Mwakilishi, amemdhalilisha Waziri, basi sheria ifanye kazi, apigwe fani au hana aende siku

kumi Chuo cha Mafunzo, ndio kwa nini amdhalilishe kiongozi wa nchi.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, watu wamekuwa na lugha za kejeli kejeli mpaka kwa maraisi wa nchi hii, kuwe na sheria zinazoweka wazi wazi watu waweze kuchukukiwa hatua ili nchi ipate kwenda na mikondo ya sheria, nchi haiwezi kwenda hivi hivi kama vile ngalawa iliyokuwa imekata tanga lazima sheria zitumike.

Mhe. Mwenyekiti, lazima vile vile tuwe na utaratibu wa Kamati za Baraza la Wawakilishi kuangalia taratibu zinazoendeshwa. Je, zinakwenda vizuri, tumekuwa na utaratibu wa kupeleka kesi Mahakamani lakini Jaji anaweza kuipiga danadana kesi hiyo miezi sita, mwaka mzima, miaka miwili, miaka mitatu, hakuna sababu. Maana wewe ukiwa umebaka, aliyebakwa yupo, watu wameshuhudia, daktari keshathibitisha, tena danadana hiyo ina maana gani. Ina maana gani sasa danadana hiyo na mimi naiomba ile kamati si vibaya kuongeza tena kifungu cha sheria cha kwamba mbakaji kama atakuwa amethibitishwa na Mahakama basi akiingia jela viboko kumi na mbili akitoka jela viboko kumi na mbili.

Hii iongozwe na nasema hivyo kwa sababu Mwalimu Nyerere alisema kwamba kuna watu hawaoni aibu kufungwa, wanaona aibu kupigwa viboko, alisema Mwalimu Nyerere hayo na mimi nakariri, na kweli ikiwa umepigwa viboko kumi na mbili umepelekwa umetoka sasa kumi na mbili unatoka. Matokeo yake ukenda kwa mkeo unaalisa vidonda unaona haya, kwamba umepigwa kwa sababu mbakaji. Kwa hivyo viboko kumi na mbili viongozwe na si vibaya katika mazingira ya kujenga utamaduni wa Wazanzibari kwa sababu tuna mambo mawili hapa tunayafanya.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, tunalinda utamaduni wetu kama Wazanzibari na pia tunalinda vizazi vijavyo, hatuwezi kuwa na taifa la mabaradhuli, lazima tuwe na taifa la nguvu kazi na njia pekee ni viboko, viboko tu sio kumfunga tu haitatosha, apigwe viboko kumi na mbili kuingia na viboko kumi na mbili kutoka tena viboko vyenyewe vile ninavyovikumbuka mimi vya sitini na nne, kumi na mbili kwa ishirini na nne ndio viboko ninavyokumbuka mimi, ehee! unapigwa wap wap unarudia tena, kinahesabiwa kimoja hicho.
Mhe. Mwenyekiti, haya mambo lazima tuyasimamie Kamati za Baraza la Wawakilishi wameibua vitu vizito katika kujenga nchi hii na lazima kamati hizi zipewe nguvu, ili serikali ipate nafasi ya kufanya mambo mazuri kwa wananchi. Serikali hii imeahidi mambao mengi chini ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi na Chama cha Mapinduzi kinarudia tena kwenye ushindani 2020, kwa vile lazima yale mema yafanywe na yale mabaya tuyaache, ikiwemo

kuweka hizi sheria kuzifanyia kazi na lazima tuhakikishe kwamba sheria zinachukua nafasi yake.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu mimi nia yangu ni kutaka kuwambia Wazanzibari wakubali kuheshimu sheria bila ya kushurutishwa, kwa vile hakuna haja ya kwamba wabakaji tuwadhibiti kwa kusuluhishana vijumbani, vijumbani, wabakaji wapelekwe Mahakamani ili huu udhalilishaji katika nchi yetu uondoke. Nna ninachukua pia nafasi hii kumpongeza sana Kamanda wa Mkoa wa Mjini/Magharibi Ndg. Hassan Nassir kwa ujasiri wake wa kumkamata Kiringo.(Makofi).

Mhe. Mwenyekiti, ahsante. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Nakushukuru Mhe. Said Soud Said Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum pia ni Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi. Waheshimiwa kabla sijamuitza Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora nilikuwa nakuomba sana Mhe. Waziri katika Kanuni yetu kuna kamati kuna jadweli la kwanza Kamati za Baraza la Wawakilishi chini ya kifungu cha Kanuni 106, mule mna kazi na majukumu ya kamati.

Kwa hivyo katika hii ripoti iliyowasilishwa hapa ya Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo basi yapo yale majukumu yake ambayo kamati inatakiwa ifanye. Kwa maana hiyo, kuna mambo mengine ambayo umeyazungumza si kazi ya Kamati hii ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo. Kwa hivyo nakuomba uipitie vizuri uone nini majukumu ya Kamati ya Kanuni hii ya Sheria Ndogo Ndogo. *(Makofi)*

Ahsante sana na sasa naomba nimwite Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora na atafuata Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote na mimi nishukuru kwa kunipa nafasi hii kidogo tu kwa muhtasari kuzungumza nukta mbili tatu zilizocheza.

Lakini nichukuwe nafasi hii pia kumshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati hii, Mwakilishi hodari, mahiri Mhe. Rashid Makame Shamsi, ina maana kapata mwalimu mzuri sana maana yake sasa hivi anafanya vizuri sana huyu. Lakini nikupongeze na wewe kuwa ni Makamo Mwenyekiti wa kamati hiyo na Wajumbe wote ambao wamo kwenye Kamati hii ya Kanuni Ndogo Ndogo.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwa upande wangu kuna mambo mawili matatu nataka niyazungumzie kwa ujumla. Kwanza nikiri kwamba kuna changamoto zimejitokeza zimeonekana na kamati yenu au Kamati yetu hii ya Kanuni, kwa vile sisi kama ni Wizara upande wetu tumepokea na kubwa zaidi limezungumzwa sana suala lile la Wakfu na Mali ya Amana hasa kwenye kanuni zake kuna lugha mbili zinatumika za Kiswahili na Kiingereza. Mimi nadhani hili neno la kimsingi na lazima tuliangalie Kanuni zetu hazindi kuwa na lugha mbili, lazima tutumie ile lugha kama ile ya taifa na pia tuipe kipau umbele. Kwa hivyo hilo tumelichukua na tunalifanyia kazi *Inshaallah* tukijaliwa na nina imani yangu kwamba hata tukija tena katika kikao cha Septemba basi marekebisho hayo yatakuwa tayari tumeshafanya yake mengi ambayo yametaajwa hapo. Niwapongeze Wajumbe kwa michango yao mbali mbali lakini na mimi nikubali kwamba naipokea ripoti hii.

Mhe. Mwenyekiti, na *Inshaallah* tukijaliwa niwapaongeze na waendelee kufanya kazi tushirikiane kwa utaratibu mzima wa kutengeneza Kanuni zetu ziwe zinafahamika vizuri. Lakini nataka nitowe wito kidogo na nishamuandikia mwenyekiti, naye kakiri baadhi ya lugha ambazo tunatumia kwenye chombo chetu hiki, tutumieni Kiswahili fasaha au sanifu na kuna maneno ambayo hayamo kwenye Kamusi la Kiswahili la Zanzibar, na hapa yanapendwa sana kuzungumzwa. Natoa wito kwamba tusiyatumie sana maneno yale kwa sababu hayakubaliki kwenye Kamusi yetu, hasa kama mwalimu kwa ruhusa yako, mimi nataka niyazunguze haya maneno mawili, wadau na kuboresha. Kwenye Kiswahili hakuna maneno hayo. Kwa hivyo badala ya kusema wadau tuseme wahusika na badala ya kusema kuboresha tuseme kufanya bora zaidi, ahsante. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Waziri wa Nchi, (OR) Katiba na Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Waziri wa Nchi, (OR) Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nichukuwe nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii lakini pili nichukuwe nafasi hii kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati hii Mhe. Rashid Makame Shamsi kwa uwasilishaji wake mzuri ambao ameufanya asubuhi ya leo katika kuwasilisha ripoti hii ya Kamati ya Kanuni.(*Makofi*).
Lakini pili niwapongeze Wajumbe kwa michango yao ambayo wametimiza majukumu yao Kikatiba na Kikanuni zetu za Baraza la Wawakilishi kutoa maoni yao juu ya jambo lolote lile ambalo linaletwa mbele ya Baraza lako tukufu Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi nina mambo machache ambayo nitapenda niyatolee ufafanuzi. Asubuhi hapa mchangiaji wa pili alikuwa Mhe. Ali Salum Haji,

umarufu lile jina unalomwita Mhe. Mwenyekiti mimi siwezi kumwita lakini namjua kwa jina la Mhe. Ali Salum Haji Mnadhimu wetu, yeye alianza kwa aya na alitufundisha sana hapa leo alitukumbusha kutuambia kwamba haya mengi ambayo utawala wa kidunia unayafanya yanatokana na kitabu cha Mwenyezi Mungu, ndivyo nilivyomnukuu mimi na nilimuelewa kwamba wapo Wajumbe ambao wamezungumzia suala adhabu, kwa maana ya faini na vifungo au kifungo, wapo waliosema kwamba unapotoza faini iwe faini tu isiwe na kifungo.

Lakini huo ni utaratibu wa kidunia katika kuweka adhabu, unaweza ukaweka faini, unaweza ukaweka adhabu, ukavitumika vyote viwili kwa pamoja au ukapewa kimoja kati ya hivyo viwili ni utaratibu wa kisheria unaotumika katika kuendesha utawala wa kibinadamu. Kwa hivyo nataka niseme nini, nataka kusema jambo lilikishaitwa adhabu haliwi rahisi, iwe faini, iwe kifungo, maana yake ni adhabu. Kitabu cha Mwenyezi Mungu kilipoweka suala la mwizi kukatwa mkono, hekma hiyo ya Mwenyezi Mungu ilikuwa inajua kwamba ukimkata mtu mkono atakuwa kilema, lakini ndio adhabu yenyewe. Na lile jengine la ukifanya zinaa ushahidi ukipatikana upigwe mawe mpaka ufe, ndio adhabu yenyewe. Kwa hivyo kitu chochote kinachoitwa adhabu hakiwi rahisi siku zote. Kwa hivyo nataka Waheshimiwa Wajumbe tulielewe hilo kwamba unapoambiwa unapewa adhabu maana hicho kitu kitakuwa kigumu kwako.

Mhe. Mwenyekiti, eneo jengine ambalo nataka niliseme kwa jumla kwamba Kanuni ni sehemu ya utekelezaji wa sheria. Kwa hivyo Kanuni ni sheria na ikishakuwepo hiyo Kanuni kuondoka kwake ama muifute ama muirekebishe. Sasa hivi katika Sheria yetu ya Serikali za Mitaa imetambua kuwepo kwa Kanuni, na Kanuni ya jumla imetungwa na hatimae *local government* kwa mujibu wa tafsiri ya sheria ile watatengeneza kanuni ndogo ndogo, lakini kanuni ya jumla imeshatungwa na hivyo hatuna budi sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tuisimamie Kanuni ile itekelezwe kwa mujibu wa utaratibu uliopo.

Jengine ninalotaka kumalizia kusema ni utaratibu wa kujibu hoja, huu ni utaratibu wetu sisi wenyewe Wawakilishi ndivyo tulivyojiwekea. Nakumbuka nilipoingia mimi Baraza la Wawakilishi 1995 Utaratibu wa Kazi za Kamati tunafanya kazi kuanzia mwezi wa Julai tunapomaliza Baraza na ripoti yake tunakuja kuiwakilisha mwezi wa Machi. Hekma yake wakati ule ilikuwa kwamba tunapokwenda kwenye bajeti, yale mengi ambayo yamefanywa na kamati Waziri anapokuja na bajeti yake awe ameyatolea ufafanuzi. Lakini ni sisi wenyewe tulioamua kwamba utaratibu huu tuundoshe, badala ya kuleta taarifa mwezi wa Machi na Waziri ajibu kwenye kikao cha Baraza, tukaamua kwamba sasa tuweke mwezi wa Septemba.

Kwa hivyo nimuombe Mhe. Suleiman Makame Ali kwamba huu ni utaratibu tuliojiwekea, tukiona sasa haufai basi ni sisi wenyewe tunaweza tukaamua. Lakini natoa *experience* yangu ya miaka hiyo kwamba ilikuwa tunafanya kazi kwenye kamati na Mawaziri wanapokuja kwenye bajeti wanatoa ufafanuzi juu ya yale mambo ambayo kamati imeyaona. Lakini Baraza hili hili ndilo lililosema kwamba aah! tunataka muda wetu maalum, sasa ni sisi wenyewe tukiamua hilo halina shida.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo niendelee kuipongeza Kamati chini ya mwenyekiti wake na kwa bahati nzuri mimi Kamati hii nimekutana nao na yale mengine ambayo yamezungumzwa, kuna marekebisho kidogo ya *era* ndogo ndogo nadhani haya tulishakubaliana kwenye kamati. Hata hivyo nataka niseme kwamba mwezi wa Septemba tutakuja na majibu yote kama Kamati ilivyopendekeza. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru sana Mhe. Waziri. Sasa naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati.

Mhe. Rashid Makame Shamsi (Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo): Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii na fursa sasa ya kuweza kufanya majumuisho madogo baada ya uwasilishaji wangu kwa ripoti ya Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo ya Baraza.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikupongeze wewe mwenyewe binafsi lakini vile vile nikupongeze kama Makamu Mwenyekiti wa Kamati yangu ya Kanuni kwa kunisaidia kupunguza baadhi ya maneno. Pia nichukue fursa hii Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote ambao wamechangia hotuba hii, hususan wale ambao Kanuni zao tumeweza kuzifanyia kazi kwa mashirikiano makubwa. (*Makofi*).

Nimpongeze sana Mhe. Maalim Haroun Ali Suleiman, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora, nimpongeze sana katika suala zima la kuweza kutukosoa katika matumizi fasaha ya lugha ya Kiswahili. Namuahidi kwamba tunayachukua na taratibu tutazoea hayo maneno, na kwa sababu Kamusi za Kiswahili fasaha tunazo kwa hiyo tutaendelea kujifunza. (*Makofi*).

Vile vile nimpongeze Mhe. Haji Omar Kheir, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ ,kwa mashirikiano yake nae lakini kwa maelezo ambayo ameyatoa ya kuisaidia sana kamati. Pia nimpongeze sana Mhe. Balozi Amina Salum Ali ambaye leo hayupo kwa mashirikiano na wote

hawa nawapongeza pamoja na watendaji wao wote wa wizara zao kwa mashirikiano waliyotupa. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, nichukue fursa hii vile vile kuwapongeza Wajumbe wote ambao wameweza kuichangia na kuifanyia haki ripoti hii ambayo ni ripoti ngumu kidogo na kwa sababu ni mara ya kwanza kwa kamati kuweza kuwasilisha ripoti hii.

Mhe. Mwenyekiti, ukweli ni kwamba Wajumbe ambao wametuchangia walijikita katika maeneo matatu muhimu. Eneo la kwanza ni kuipongeza Kamati, hivyo kwa niaba ya kamati yangu nachukua pongezi zote ambazo Wajumbe wametupa na niwashukuru sana kwa uungwana wao wa kuona umuhimu wa kamati hii na utendaji wa kazi zao.

Eneo la pili lilikuwa ni eneo la maoni ya Wajumbe kutuunga mkono kwa yale ambayo tumewasilisha. Kwa hivyo tumeyapokea maoni yao ndugu Wajumbe na mmetuunga mkono, kwa hivyo tunakupongezeni kwa kutuunga mkono juu ya hayo. Mhe. Mwenyekiti, ni ushauri kwa hiyo niseme ushauri na mapendekezo ambayo wameyatoa basi tutayafanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu ya kanuni katika ripoti hii imechangiwa na wajumbe 15. Wajumbe 10 waliichangia kamati hii kwa kusema moja kwa moja katika ukumbi na Wajumbe 5 walichangia kwa maandishi. Kwa niaba ya kamati naomba nichukue fursa hii kuwatambua wajumbe hao. Kwa wale ambao wamechangia moja kwa moja ni.

1.	Mhe. Rashid Makame Shamsi	Mwenyekiti wa Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo
2.	Mhe. Suleiman Sarahan Said	
3.	Mhe. Ali Salum Haji	
4.	Mhe. Ame Haji Ali	
5.	Mhe. Miraji Khamis Mussa	
6.	Mhe. Panya Ali Abdalla	
7.	Mhe. Suleiman Makame Ali	
8.	Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum)	
9.	Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora.	
10.	Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ.	

Mhe. Mwenyekiti, hawa ndio waliochangia kwa kusema moja kwa moja, lakini kwa wale ambao wamechangia kwa maandishi Wajumbe 5 walikuwa ni.

1. Mhe. Mohammed Mgaza Jecha
2. Mhe. Ussi Yahya Haji
3. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma
4. Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa) na
5. Mhe. Ali Suleiman Ali

Mhe. Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuwapongeza Wajumbe wote waliotuchangia katika ripoti yetu na nawashukuru sana.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, sasa nimalizie katika baadhi ya maoni ambayo wameyatoa Waheshimiwa Wajumbe. Waheshimiwa Wajumbe walijikita kuweza kuungana na kamati ipewe mafunzo zaidi kwa hiyo tunashukuru. Vile vile walizungumzia suala la lugha wametuunga mkono katika hilo, lakini umuhimu wa uwepo wa Kamati hii ya Kanuni, kwamba ni kamati muhimu ambayo itaisaidia Baraza katika kutekeleza yale majukumu yake ambayo Baraza inayakasimu kwa Mawaziri au kwa vyombo vyengine katika suala zima la sheria. Mhe. Mwenyekiti, lakini suala la majukumu na hili ambaye wewe ni Makamu wangu wa Kamati umenisaidia sana kuweza kutoa hasa majukumu ya kamati.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, majukumu makubwa sana pamoja na majukumu sita ambayo yametajwa katika Kanuni, lakini jukumu kubwa sana la kamati hii ni kuweza kupitia Kanuni, kuweza kuchambua na hatimae kuweza kutoa mapendekezo kwa taasisi husika.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Said Soud Said tunapokea sana ushauri wake na mapendekezo na aliitaka kamati iweze kuripoti juu ya kesi ya kuzama kwa meli, lakini kutokana na majukumu yetu basi hatuwezi kuingia huko. Lakini suala zima tunalotazama sisi ni uchambuzi wa Kanuni. Vile vile Mhe. Said Soud Said alizungumzia juu ya Kamati kuweza kutazama mambo madogo madogo ambayo yataweza kuimarisha utawala bora katika nchi hii. Sasa tunapochambua Kanuni maana yake tunazisaidia sheria hizi ziweze kutekelezeka kwa njia bora zaidi. Hilo ni sehemu ya huo utawala bora ambao Mhe. Waziri amezungumza.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia Mhe. Waziri amezungumzia suala la baadhi ya wafanyabiashara kuleta ubaguzi wanapotoa huduma. Nimwambie tu Mhe. Said Soud Said kwamba juzi juzi tulipitisha sheria ya ushindani halali wa biashara na kumlinda mtumiaji. Kwa maana hiyo wote hawa ambao wanatoa biashara kwa ubaguzi au wanazuia biashara, ili wananchi wapate tabu basi sheria hii baada ya kutiwa saini itawaandama.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo nirudie tu tena kuwashukuru waheshimiwa wote ambao wametuchangia hotuba hii, na niombe tu kwamba waendelee na

moyo huu wa kuichangia kwa sababu hii ni kamati mpya kabisa, majukumu yake ni mazito na ina changamoto za Kikanuni.
Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo basi naomba kutoa hoja. Ahsante sana. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati. Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa sasa naomba niwahoji wanaokubaliana na hoja hiyo, wanaokataa, wanaokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Waheshimiwa Wajumbe na mimi nichukue nafasi hii kuwashukuru sana Wajumbe wote ambao mmechangia, lakini pia niipongeze kamati ikiongozwa na mwenyekiti kwa ripoti yao na imani yangu kwamba Mawaziri wote wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambao wanaleta sheria hapa Barazani ili kuzipitisha basi kama kuna vile vifungu ambavyo vinahitajika kutungiwa Kanuni, basi wafanye jitihada hizo ili kuifanya ile sheria iweze kutekelezeka.

Nawashukuru sana lakini pia kwa mujibu wa kazi zetu za leo zilizopangwa katika *order paper* tumezimaliza. Kwa hivyo naomba niahirishe kikao hiki mpaka kesho saa 3:00 asubuhi.

(Saa 7:52 mchana Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 27/02/2018 saa 3:00 asubuhi)